- Watu wote walipuhuza kumuheshimu Mungu, walikuwa inje ya safina na wote waliangamia pamoja na viumbe vyote vyenye kuwa na uhai navyo vilikufajapo hiyo Nuhu na jamaa lake walikuwa na zambi Asili kutoka kwa adamu na Eva walimuheshimu Mungu na kuamini agano lake la kuwaleteya mukombozi kuwaokowa katika utumwa wa shetani

- Kwa sababu Nuhu alikuwa kwa Mungu, alimuaminiya na kumuheshimiya Mungu, Mungu alimuokowa na akamukubali kama mwenye hakukuwa na zambi.
- Mungu alitiya upinde wa muula juu kama vile ishara ya kuonesha, ya kama hatahangamiza tena wanadamu kwa maji.
- Nuhu alicinja nyama akatoleya Mungu sadaka, akamushukuru kwa ku muokowa yeye na jamaa yake kwa kifo.
- Hadisi hiyi ya Nuhu ni mufano wa Mukombozi atakaye kuja kuwaokowa wote waliyo mwamini ili wasihingiye katika ziwa la moto.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

EZEKIELI 18 :32

Maulizo ya uchunguzi

1. sababu gain watu wakati wa Nuhu walifanya zambi? *Kwa sababu walizaliwa ni wenye zambi na walimufata shetani.*
2. Ni na muna gani Mungu alipanga kuangamiza maisha yote mudunia? *Kwa kuleta mafuriko*
3. Ni nani aliyehokolewa na Mungu na kutokukumbwa na maji? *Nuhu*
4. Sababu gani Mungu alimuokowa mtu huyo na jamaa lake? *Ni kwa sababu walimwamini na kumuheshimu Mungu.*
5. Je Mungu aliwapatiya wakati wa kumurudiliya na ku muamini ? *ndiyo miaka 120*
6. Mungu alifurahiya kuzama wenye zambi ? *hapana Mungu hapendi mtu yeyote kukufa.*

SOMO LA 16

IBRAHIMU NA ISAKA

Shauri kwa mwalimu :

Somo hili ni lazima sana sababu ni mufano wa yesu kwa ni alikuja kufa mahali petu utawakumbusha wanafunzi hadisi hiyi kiisha ndani ya somo.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mwanzo 11 :1-9
Mwanzo 12 :1-5
Mwanzo 15 :1-6,13-14
Mwanzo 18 :1-15
Mwanzo 22 :1-19
Waebrania 11 :8-12
Waebrania 11-17-19

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Fundisha nafasi hiyi kwa wanafasi

- Miaka mingi imepita tokeya maji ya gharika yalipokeya, na wakati wote huo watu waliongeya luga moja.
- Mungu alipenda watu waishi katika kila sehemu ya dunia, Mungu akapatiya wanadamu luga mbalimbalikusudi watawanyike duniani na wahijaze aliwa haidiya
- Mungu hakusahau mupango wake wa kutuma duniani, mukombozi ambaye aliwahaidiya.
- Mungu alimuhita mwanadamu mwenye kuitwa ibrahimu naye alikuwa anishi kati ya wakosefu, na akamwambiya atoke mahali hapo aende mu inchi yenye atamuonesha.
- Abrahamu, alimuhaidi kwamba :
    1. nitakufanya baba wa watu wengi
    2. Nita kubarikiya na kulifanya jina lako kuwa kubwa
    3. Kwa kupitiya weye mataifa yote ya duniani yatabarikiwa (mukombozi, aliye haidiwa na Mungu ni wa ukoo wa Abrahamu)
    4. Ukoo wako watababwa mu utumwa mu inchi ingine miaka 400.
- Mungu aligeuz jina la Abrahamu likawa Ibrahimu na maana ya jina hilo ni Baba wa mataifa na jina la mke wake aliitwa sarai ila akaitwa sara maana yake mama wa mataifa.
- Ibrahimu na sara wote wa wili walikuwa wazee sana hawa kuzaa mtoto
- Hakuna lenye aliwezekani kwa Mungu, Mungu alimupa Ibrahimu ahadi kama anamupa mutoto mwanaume.
- Ibrahimu alimuamini Mungu, na Mungu akamupokeya kama mtu asiyekuwa na zambi. Mwanzo 15:6,
- Wakati sara alipo fikisha miaka 90 alimzaa Isaka
- Ibrahimu alimpenda sana Isaka
- Mungu alipenda kumujaribu Ibrahimu siku moja kusudi aone jinsi gani Ibrahimu anampenda na jinsi anamuamini.

- Mungu alimuambiya Ibrahimu amkamate Isaka mpaka juu ya mulima ili amtoe sadaka.
- Ibrahimu akamuamini Mungu na kumuheshimiya , akakubali kwamba Mungu hata muhua IsakaMungu alipendezwa na imani yake Ibrahimu.
- Mungu akukubali Ibrahimu amuhuwe Isaka.
- Kondoo ili chinjwa nafasi ya Isaka
- Isaka hange jiponyesha, Mungu alimuparesha kama vile alivyo muokowa Nuhu munamo miaka mingi mbele ya Isaka.
- Mungu akusahau mpango wake wa kutuma mukombozi mwenye alihaidi naye mkombozi ni wa kutoka mu uzao wa Ibrahimu Isaka.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Waebrania 11:6

Maulizo ya uchunguzi

1. Taja jina la mtu mwenye Mungu alimuhita ili akae mu inchi ingine? *Abrahimu*
2. Je Ibrahimu alimuamini na kumuheshimu Mungu? *Ndiyo*
3. Ni ahadi gani yenye Mungu alimuagiza Abrahamu ?
    1. *nitakufanya baba wa taifa*
    2. *nitakubarikiya na kufanya jina lako likuwe likubwa.*
    3. *kupitiya wewe mataifa yote yatabarikiwa.*
4. Mtoto wa Ibrahimu aliitwa nani *? Isaka*
5. Kwa nini Mungu alimupenda Ibrahimu ? *kwa sababu Ibrahimu alimuamini na kumuheshimu Mungu*
6. tutaweza fanya aje ili tumupendeze Mungu ? *kwa kumuamini na kumuheshimiya Mungu.*

SOMO LA 17

MUNGU ANAJENGA TAIFA LAKE NA ANAMWITA MUSA

Shauri kwa mwalimu :

Mungu alitumia wakati wa kutosha huko misri akiliongoza taifa lake ambao walitoka katika jamaa la yakobo (walikaribiya watu 70) wakafika watu milioni 2 Musa aliwakombowa hao watu kuwatowa utumwani huko misri nao ni mufano wa jinsi yesu alivyotukombowa kutoka katika maisha ya zambi chini ya utawala wa shetani.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mwanzo 25 :19-20
Mwanzo 25 :24-26
Mwanzo 28 :12-14
Mwanzo 32 :28
Mwanzo 37 :34,12-36
Mwanzo 42 :1-8
Mwanzo45 :1-11
Kutoka 1,2,3

Rudilia maulizo ya somo lililo pita pamoja na wanafunzi

Fundisha nafasi hiyi kwa wanafunzi

- Isaka alimuowa mwanamke aliye hitwa Rebeka walipata watoto wanaume wa mapasa, umoja aliitwa Yakobo ungine aliitwa Esau Esau alizaliwa mbele ya yakobo.
- Mungu anajuwa kila kitu sababu alijuwa kama yakobo atamuamini mbele ya yakobo kuzaliwa Mungu akamuchaguwa yakobo awe babu wa mkombozi
- Yakobo alimuheshimu Mungu, na Mungu akamupa ahadi aka mupa ahadi kama vile alivyo mpatiya Ibrahimu na Isaka Mungu alimupatiya jina lake Israeli badala ya yakobo. Yakobo alikuwa na watoto wanaume kumi na mbili 12 watoto hao waliitwa wana wa Isareli Mtoto mwenye yakobo alipenda sana alihitwa Yusufu.
- Ndugu zake na yusufu walimuoneya wivu wakamuhuzisha kwa wafanya biashara wakampeleka akaenda kuwa mtumwa mu inchi ya kigeni ya misri
- Miaka mingi ilipita kukatokea njaa katika inchi yenye wa Israeli walihishi ndani.
- Israeli akawatuma watoto wake kwenda kuuza chakula misri.
- Wawalikutana huko na ndugu yao Yusufunaye sasa alikuwa ni mtu mkubwa katika inchi ya misri
- Yusufu aliwasemehe wadugu wake mambo yote yenye walimufanyiaka akawaita wote na familia zao ili waende kuishi naye kule misri
- Watu 70 wenye walitoka mu familia ya yusufu walikuja kuishi misri

- Waliikaa misri miaka 400 na wakaongezeka mpaka wakafika watu milioni 2 wakawa taifa la mukubwa lenye Mungu alimuahidiya Ibrahimu.
- Farao mufalme wa misri alipata wasiwasi kwa kuona jinsi Hesabu ya wana wa israeli wenye kuishi misri inakuwa kubwa sana.
- Aka wafanya kuwa watumwa na kuwa shurutisha kufanya kazi za nguvu kwa kujenga miji yake mikubwa, sawasawa na vile Mungu alivyo mwambiya Ibrahimu kwa myaka mingi yenye ilipita.
- Aka hamuwa kuhuwa watoto wa kiume wote wa waisraeli : shetani alimutumikisha farao ili ajaribu kupinga mupango wa Mungu
- Mupango wa Mungu ilikuwa ni kuwaokoa wa israeli kusudi mukombozi apate kutokea katika taifa hilo.
- Hakuna kinacho weza kupinga mpango wa Mungu
- Mungu akamuokowa mtoto mumoja mwenye aliitwa Musa Mungu akamuchaguwa kamani yeye mwenye atawakombowa wa israeli kutoka katika utumwa wa farao.
- Mama mama yake ya musa alimuficha ndani ya kikapu na akamuweka katika mtoni nile akiwa ndani ya hicho kikapu
- Binti farao akamulogota Musa akalelewa na kukuwa katika nyumba ya mufalme akajifunza kusoma na kuandika, na akapata elimu nzuri sana kama wa misri
- Kiisha Musa kuwa mtu mzima aliona jinsi wa misri walivyo kuwa wakiwafanyia mubaya wana wa israeli akakasirika na akamuhuwa mwana jeshi umoja wa ki misri.
- Musa alipata wasiwasi akaogopa kwamba Farao atamuhukumu, kiisha akahamua kukimbiya kutoka misri
- Akajikusanyana kuikaa imara mu inchi ya jangwa miaka 40
- Siku moja Mungu alihongeya na Musa kupitiya mu kichakachaka moto, aka muambia arudiye aende kuwakombowa waisraeli kutoka katika utumwa wa Farao
- Musa aluhamini Mungu na akaheshimu sheria zake akakamata ndugu yake Hroni wakarudiya Msri.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Maulizo ya uchunguzi:

1. Mungu alimupa yakobo jina gani? *Israeli*
2. ni inchi gani yenye aliwatuma watoto wake kwenda kutafuta chkula? *Misri*
3. kwa nini Farao alihamuwa watoto wanaume wa wa israeli? *kwa sababu alikuwa anawaogopa wa israeli na tena shetani alimutumikisha ili ajaribu kupiga mupango wa Mungu wa kuleta mukombozi*

4. Mtoto mwenye binti Farao alilogota mu mtoni alihitiwa nani? *Musa*
5. Musa alikomaliya wapi? *Katika nyumba ya mufalme kama mtoto wa mufalme*
6. Kiisha Musa kuwa muzima, Mungu alimuambiye afanye nini? *Alimuambiya arudi misri kuwakombowa waisraeli kutoka katika utumwa.*

SOMO LA 18

MUNGU ANAONYESHA NGUVU ZAKE

Shauri kwa mwalimu

Hiyi ni hadisi muzuri sana yenye kuonyesha nguvu na huruma za Mungu kwa wale wanao muamini piya inahonyesha kasirani ya Mungu kwa wale wenye hawatasikiliza maonyo yake. Damu yenye ilipakaliwa kunguzo za milango, inanyesha mufano wa damu ya yesu jinsi inavyowalinda wale wote wanao mukubali yesu kuwa mwokozi wao kwa kuwatowa kwenye hukumu ya zambi.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Kutoka 5:1-2
Kutoka 6:1-8
Kutoka 11:1-7
Kutoka 12:1-8
Kutoka 12:12-13
Kumbukumbu 7:7-10
Kutoka 7: 1-7
Zaburi 105:1-38

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Fundisha nafasi hiyi kwa wanafunzi.

- Musa alirudiya misri kama vile Mungu alivyo muambiya lakini Farao alikatala kuwapa ruhusa ya kutoka mu inchi yake
- Faraona watu wa misri wao hawakuamini na kuabudu Mungu umoja wa kweli
- Wa misri walikuwa wenye akili na wenye pesa nyingi walijenga manyumba mazuri na miji mizuri, walikuwa na jeshi lenye nguvu na wakawa hodari
- Shetani aliwasababisha kuomba miungu ya uongo wakasadiki kama jua ni Mungu wao, mutoni ni mungu,nyota ni mungu, waliabudu ata machura walitosha wa toto wao kama sadaka kwa miungu hiyo ya uongo.
- Walikuwa wanaabudu vitu vyenye Mungu aliumba,kuliko kumuabudu Mungu mwenyewe
- Wakati wakati unafika wa Mungu kuonyesha nguvu zake na kuwahukumu watu hao wabaya
- Mungu alimutuma Musa kufanya Ishara za nguvu sana kwa kuonyesha nguvu zake zenye kupita ile miungu ya uongo, mpaka farao akakubali kuwapa ruusa wana wa israeli kutoka misri.

- Mungu aliyageuza maji yoye ya inchi ikawa damu, kisha akaleta ma milioni ya ma chura yakafunika inchi, kisha akaleta vidudu vidogo vidogo na ma inzi kisha akagonjwesha wanyama wote wa misri na wa misri wakawashwa mwili mzima.
- Mungu akanyesha nvuwa ya majiwe yenyekuwa mungurumo na kali akaleta nzige , na akafanya inchi yote ikawa na giza kubwa muda wa siku tatu, hata alifanya hayo yote Farao aliendelea kukataa kumupa ruhusa na wa israeli
- Mwisho, Mungu alifanya kitu kimojacha ajabu aliambiya waisraeli wa chinje kondoo dume anaye nona na damu yake wapakae kwenye visingiti vya milango ya nyumba zao.
- Usiku huo Mungu alituma malaika wa kifo katika inchi iyo ya misri wale wote wenye hawakuheshimiya sheria za Mungu, watoto wao wa kwanza na wa wanyama wao wote walikufa
- Ku mwisho Farao aliwapa ruhusa wa israeli kutoka , watu karibu milioni2 walienda nyuma ya Musa wakitoka inje ya Misri
- Kila wakati Mungu anaokowa watu wenye kuwa na imani ndani yake yaani wanao muamini na kumuheshimu.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Nahumu 1:7

Maulizo ya uchunguzi

1. Farao aliamini Mungu umoja wa kweli aliye hai? *Hapana*
2. Ni Mungu gani yenye wa misri walikuwa na abudu? *Miungu ya uongo, mungu jua, mungu mtoni, mungu chura, n.k.*
3. Taja ishara mbili yenye Mungu alifanya kwa kuonesha farao nguvu zake? *Aligeuza maji kuwa damu, alijaza vyura vikafunika uso wa inchi.*
4. kisha Mungu kufanya hivyo, je Farao aliwapa ruhusa waisraeli kutoka Misri? *Hapana.*
5. Mungu aliwambiya waisraeli watumikishe nini ile damu ya nyama yenye walichinja? *Kuipala ku vizingiti vya milango ya nyumba zao.*
6. kitu gani kilitokea kwa jamaa zenye hazikuheshimu sheriya za Mungu? *Mzaliwa wao wa kwanza na wa mnyama wao walikufa.*

SOMO LA 19

MUNGU ANAWAHUDUMIA WAISRAELI JANGWANI

Shauri kwa mwalimu :

Somo hili linaonyesha mapenzi ya Mungu, uchunguzi wake na msaada wake kwa wale wote wanao muamini piya inaonyesha mateso yenye iko anapata wakati murefu kwa wa vumiliya wale wenye hawa muamini.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Kutoka 13:17-18
Kutoka 14:5-31
Kutoka 16:1-2
Kutoka 17:1-7
Kutoka19:1-6
Zaburi 105:39-45

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Fundisha nafasi hiyi kwa wanafunzi

- Musa na wana waisraeli walikuwa hawajaenda muda murefu sana mbele ya Farao kugeuza uamuzi wake alianza kwamba ni sababu gani aliwapa ruhusa waisraeli kutoka mu inchi yake.
- Farao na jeshi lake lote walianza kuwafata wa israeli nyuma.
- Waisraeli walihingiya mu mutego wakiwa katikati ya jeshi la Farao na Bahari
- Mungu ni mwenye haki kwa yote yenye anasema na ana fanya hakuna chenye kuwa kigumu kwa Mungu . Mungu alifanya ishara kubwa na akatoa upepo mukali bahari ikafunguka na Mungu akawapa ruhusa waisraeli wakapita mahali penye kukauka katika bahari kwa usalama wakienda upande mwengine wa bahari
- Wa misri walipima kuwafuatiya kwa nyuma, Mungu akahifunga tena bahari ndipo Farao na jeshi lake lote wakaangamizwa na bahari
- Mungu ameokowa taifa lake na anaenda sasa kuwapeleka katika inchi yenye alimuahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo
- Kiisha siku kidogo mu jangwa wa israeli walianzapata kiu, njaa na wakaanza kumsirikiya Musa na kumuhuliza sababu gani aliwatowa katika inchi ya misri huko misri walikuwa na vyakula vingi na maji, walikuwa na wasi wasi kwamba wangekufiya mujangwa.

- Walikuwa waliisha kusahahu yote yenye Mungu amekwisha wafanyiya hawaku sadiki kama Mungu angeweza kuwasaidiya tena.
- Mara ingine Mungu alionyesha upendo wake kwao, kila siku aliwaleteya nyama wakakula na akawapatiya chakula bora chenye walikusanya chini kila siku asubuhi chakula hicho walikihita ”mana”
- Ali wapatiya maji kwa kuambia Musa apige fimbo yake juu ya mwamba Musa aliheshimu na maji ya katoka mengi katika mwamba
- Hakuna kisichowezekana kwa Mungu aliwapatiya maji na chakula watu wakupita milioni 2 pamoja na wanyama wao.
- Kiisha miezi tatu waisraeli walifika kwenye mulima wa sinai na wakahikala huko mwaka ummoja, ni hapo Mungu alimupatiya Musa Amri za Mungu na sheriya zake.
- Kwa kutumiya haki aliwachunga waisraeli na akawapatiya kila chenye walipenda

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Zaburi 97 :10

Maulizo ya uchunguzi:

1. Mungu alifanya nini kwa kuwako mbowa israeli kutoka kwa jeshi la Farao? *Alilifunguwa bahari ili waweze kupita*
2. unawaza Mungu angewaachiliya waisraeli wakufe na njala na kiu mujangwa?*hapana*
3. aliwapatiya chakula namuna gani? *Aliwaleteya ndege na mana kila siku kama chakula chao*
4. maji waliyapata wapi? *Katika mwamba*
5. ni watu ngapi wenye Mungu alikulisha mu jangwa? *Karibu milioni 2*
6. je Mungu anatupatiya tunavyotaka wakati wenye tuna muamini na kumuheshimu? *Ndiyo.*

SOMO LA 20

MUNGU ANAMUPATIA MUSA AMRI ZAKE.

Shauri kwa mwalimu.

Watu wengi wanafikili kama watakubaliwa na Mungu kwa sababu wanashika amri za Mungu. Hiyo siyo kabisa. Sheria zilitolewa wakati wa agano la kale.ilikuwa kuwaonyesha watu ukamilifu wa Mungu na kuwa wana muhitaji mukomboei (Yesu) atakayewaokoa. Wao ni wazaifu na hawawezi kujiokoa peke yao, lakini ni lazima tujikaza kuzitii hizi amri kwa sababu tunamupenda Mungu na tunataka kumpendeza.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Kutoka 20, 1-17,
Matayo 5, 17-20,
Kutoka 24, 12-18,
Wagalatia 3.
Waefeso, 2, 8-9.

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Wafundisha wanafunzi sehemu hii.

- Wakati waisraeli walikua wamefanya kambi kwa mulima wa Sinaï, Mungu alimuita Musa akutane naye juu ya mulima.
- Mungu alimupa Musa amri na sheria apate kuwafundisha waisraeli.
- Mungu mwenyewe aliandika Amri hizo kwa vipande viwili vya majiwe:

  Amri ya 1. Mimi ndimi Bwana Mungu wako usijifanyie miungu mingine.
  Amri ya 2 : Usiabudu kitu kingine chochote isipokuwa Mimi
  Amri ya 3: Usitaje bure jina langu
  Amri ya 4 : Ukumbuke siku ya saba. Mtu asifanye kazi siku ile
  Amri ya 5: Uwaheshimu baba yako na mama yako
  Amri ya 6: usiue
  Amri ya 7: usizini
  Amri ya 8: usiibe
  Amri ya 9: Usisemi uongo
  Amri ya 10: Usitamani chochote kilicho mali ya jirani yako.

- Mugu aliwapa waisrei sheria nyingine nyingi
- Sheria hizi zilitolewa kwa sababu Mungu alitaka watu wake kuwa tafauti na mataifa ya wapagani yaliyo wazunguuka.
- Mungu ali wataka waisraeli kuwaambia mataifa mengine habari zake nao wapate kumwamini Mungu mumoja wa kweli aliye hai.
- Mataifa mengine yote yalikuwa yakiabudu miungu ya uongo kama wamisri!
- Mungu ni mutakatifu na mukamilifu. Sheria zake ni ngumu kuzishika.
- Kama watu watavunja hata amri moja,watakuwa wakosaji kama vile wenye kuvunnja zote kumi.

- Mungu alitumia sheria kuwaonyesha watu namna yeye alivyomkamilifu na ginsi gain watu tulivyo wenye zambi.
- Sheria zilizotolewa ili watu watambue kwamba wao ni wakosefu na kuwa hawawezi kijiokoa wenyewe kwa kujikaza kuzitii tu sheria. Ni kwa kuamini Mungu kama Abedi. Noa, Abrahamu, Isaki, yakobo na Musa walivyo fanywa wenye haki mbele ya Mungu.
- Walihitaji mukombozi ambaye ataziharibu nguvu za shetani, atalia zambi zao na kuwatengenezea njia ya kurudi katika familia ya Mungu.

Mungu ni mwaminifu na kila mara hutimiza ahadi zake. Muda wa kuja mukombozi ulikuwa umekaribia.

Aya za kukumbuka ambazo mwalimu anatakiwa kuwafundisha kwa kuhakikisha ushiko kiisha somo: Yeremia 2, 10.

Maulizo ya ukaguzi:

1. Taja amri tatu zozote kati ya amri kumi za Mungu: *Usiibi, usiseme uongo, uwaheshimu baba na mama yako.*
2. Kwa nini Mungu aliwapa waisraei sheria zake? *Kuwaonyeshanamana alivyo mutakatifu na ginsi gni watu walivyo wenye dhambi.*
3. Je umewahi kuvunja sheria yoyote kati ya hizi amri za Mungu
   *Ndiyo, tunakuwa tukizivunja mara nyin*gi.
4. Ni malipizi gain itakayotolewa kwa wasiomutii Mungu? *Kifo katika ziwa la moto*.
5. Je, watu wote watendao zambi watatupiwa katika ziwa la moto*? Ndiyo, sababu kila mtu anayevunja sheria za Mungu atastahili hukumu*
6. Ni nani anayeweza kutuokoa katika hukumu ya Mungu? *Ni Mungu peke yake.*

SOMO LA 21

MUNGU ANAMUPA MUSA MAAGIZO KWA AJILI YA MASKANI YAKE.

Shauri kwa mwalimu:

Wanafunzi lazima wafahamu ya kama damu ya munyama hahiwezi kuwaondolea zambi zao tena. Mugu aliwaambia watu wafanye hivo wakati wa Agano la kale. Na kutambua kama Yesu atawalipia zambi zao wakati ujao. Kama vile mwanakondoo alivyo kufa kwa nafasi ya Isaki, na hivyo ndivyo Yesu alivyokufa kwa nafasi yetu.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Kutoka 25: 8-9,
Kutoka 26: 31-33
Kutoka 40: 34-35
Kutoka 25: 17-22
Waroma 3:25
waebrania 9
Kutoka 39: 32-43
waebrania 8:1-6
Waebrania 10:1-16.

Rudilia maulizo ya somo lilipita pamoja na wanafunzi

Uwafundishe wanafunzi sehemu hii:

- Mungu aliwapa waisreli sheria zake. Alijuwa kama hawa taweza kuzitimiza zote
- Mukombozialikuwa bado kuja. Mungu akatengeneza njia ya kuweza kuwaondolea zambi zao.
- Abeli, Noa, Abrahamu, Isaki, yakobo na Musa wamekuja kwa Mungu kwa njia ya hii ya upatanisho. Sasa Mungu anatoa maagizo kwa taifa lake lote kuja kwake kwa njia hii.
- Ni njia hii ya upatanisho isingesimamishwa kiisha mkombozi kuja.
- Walitakiwa kuja kwa Mungu kwa njia zenye waliwaambia.
- Sheria za Mungu ziliwaonyesha kama wao ni wenye zambi na kama hawana uwezo wa kujiokoa wenyew, ni Mungu peke anaweza kuwaokoa na hukumu ya kutupwa katika ziwa la moto.
- Mungu alimupa Musa maagizo ya kutengeneza hema ya kukusanyika aliyoita maskani kama vile Noa kutengeneza Safina.
- Mungu ni roho na kujifunua kwake kungeonekana katika maskani, kama mwangaza.
- Maskani hiyo ingekuwa na vyumba viwili: mahali patakatifu na mahali patakatifu pa takatifu.
- Katika szhzmu takatifu sana, palikuwa na sanduku kubwa lililotengenezwa kwa mbao na kufunikwa kwa zahbu. Upande wa juu wa sanduku kuliwekwa sanamu mbili za malaika zilizo tngenezwa kwa zahabu.
- Mara moja kila mwaka kuhani mkuu alicinja mnyama dume na kumwangia damu ya mnyama huyo kwenye sanduku katikati ya sanamu zile mbili.
- Mungu alikubali damu hii kuwa ondoleo la zambi za watu hawa kwa muda wa mwaka moja tu.
- Kifo cha munyama huyu kilikuwa mufano wa mukombozi ambayeangekuja siku zitakuja baadaye kuchua azabu ya zambi zao.

- Mchungaji mkuu alikuwa kurudia kufanya hivyo mwaka baada ya mwaka kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya taifa lote la Israeli.
- Kila siku watu walikuwa wakija pale kwenye hema na kumupa kuhani wanyama au ndege kwa ajili ya sadaka kwa Mungu.
- Njia hii iliyokuwa picha (mfano) ya kuja kwa mwana wa mungu ilitumika kwa muda wa miaka 1500 mpaka mukombozi alipokuja.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Waebrania 10:4.

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Je Mungu alitegemea kwamba Waisraeli watakuwa na uwezo wa kuzitii sheria zake zote? Hapana.
2. Ni majina gain viliitwa vyumba viwili katika maskanni yale?
- Mahali patakatifu na mahali patakatifu pa patakatifu.
3. Ni nini ilikuwawamo ndani ya chumba cha mahali patakatifu pa patakatifu?
- Sanduku la mbao lililozunguushwa zahabu na sanamu mbili za malaika zilizotengenezwa kwa zahabu.
4. Ni nin kuhani mkuu alitakiwa kufanya kila mwaka?
- Alitakiwa kuchnja munyama na kunyunyiza damu ya munyama huyo kwenye sanduku katikati ya sanamu zilz mbili.
5. Je damu ya munyama inaweza kulipa deni ya zambi? Hapana.
6. Waisraeli wangesimamisha kutoa sadka za wanyama mpaka wakati gani¸pale mkombozi alipokuja.

SOMO LA 22.

MATAYARISHO YA MUKOMBOZI.

Shauri kwa mwalimu.

Mungu aliruhusu kuuawa kwa waisraeli wote wenye hawakumwamini,tena alikataa wasiingie katika inchi ya ahadi; kama vile wakati wa Noa,hakuwaruhusu waingie katika safina wale wote wasiokuwa na imani kwake. Hata sisi vile vile tunatakiwa kumwamini Mungu kwa sababu ya kupona kwetu na hiyo tutaweza kuingia katika ufalme wa Mungu.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Kumbukumbu la torati 1:19-40
Waamuzi 2: 14-16
Yushua 1:1-11
1Samweli 8:19-22.
Luka 3:1-20.

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi.

Wafundishe wanafunzi sehemu hii:

- Wengi kati ya waisraeli amao Mungu aliwatoa Misri wasioamini wala kutii Mungu. Walikuwa walikwisha kusahau maajabu yote Mungu aliwafanyia.
- Hawakuamaini kama Mungu ataweza kuwapa ile inchi aliyo muahidia ababa yao Abrahamu.
- Mungu alikasirishwa sana na kule kukosa kuamaini kwao.
- Akawaacha wazunguuke zunguuke na kuishi katika jangwa miaka 40, mupaka pale wote walikuwa hawamwamini walikufa!
- Kiisha miaka 40 kupita, Musa alikufa, yoshua akawaongoza waisraeli mupaka kufika katika inchi ya ahadi.
- Kulikuwa mataifa mengi ya watu waovu sana walio kuwa wakiishi katika inchi ile.
- Mungu aliwasaidia watu wake kushinda vita juu ya mataifa haya maovu. Inchi ile inaitwa siku hizi Israeli.
- Mungu amejitengenezea taifa, akawapa sheria zake na inchi.
- Mapenzi ya Mungu ilikuwa yeye awe mutawala na mufalme wao kusudi mataifa yote a duniani wamwamini Mungu mumoja aliye hai.
- Kila kitu kikawa kimetayarishwa kwa sababu ya mukombozi aliye ahidiwa.
- Miaka mingi ikapita na mambo mengi yakatokea kwa nyakati hizo zote. Mungu akawaweka waamuzi na akawapatia madaraka ya kuliongoza tafa lake, lakini waisraeli hawakufurahia kuongozwa na Mungu.
- Walitaka wapate mufalme wa kuwatawala kama vile ilikuwa kwa mataifa mengine yaliyo wazunguuka,
- Sauli, Daudi na Salomoni ndiyo walikuwa wafalme watatu wa kwanza wa Israeli. Salomoni akajenga hekalu nzuri sana mujini Yerusalemuliwe pahali pa hema ya kukutania.

- Wengine kati ya wafalme walimuheshimu Mungu na wengi wao hawakumuheshimu.
- Wafalme hawa wabaya waliwaongoza watu kuabudu miungu ya uongo kama mataifa yaliyowazuunguka.
- Nyakai hizo zenye wafalme hwa wabaya walitawala Israeli, Mungu alituma manabii wengi kuwaongoza na kuwaonya waisraeli pale walipomuasi Mungu.
- Isaya ni mumoja wa manabii hao. Aliwambia waisraeli mambo mengi kuhusu mukombozi. Aliwambia waisraeli mamabo mengi kuhusu mukombozi aliyeahidiwa kusudi atakapokuja wapate kumutabua.
- Pia, Mungu aliruhusu mataifa mengine yenye nguvu kupigana na Israeli wakati ilipoasi;
- Mungu akamutuma nabii mumoja wa mwisho kuwaonya watu wake na kuwabadilisha mwenendo wao kusudi wamwamini na kumutii Mungu.
- Nabii huyu aliitwa Yohana.
- Yohana aliishi katika jangwa na likuwa maskini lakini Mungu alimutumia kuwaambia watu kujitayarisha kwa kupokea mukombozi aliyeahidiwa.
- Watu wengi waliamini ujumbe wa yohana mubatizaji na wakabatizwa naye katika mutoni wa Yordani.
- Wakati sasa ukatimiya. Ni nani huyu mukombozi aliyeahidiwa? Atazliwa wapi? Na jina lake ataitwa nani.
- Je atakuwa mufalme mkuu? Atakuwa tajiri na mwenye uwezo mukubwa? Atawaokoa waisraeli ktioka kwa maadui wao?
- Haya ni maulizo yenye kila mumoja alikuwa akiuliza.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Yohana 1:23.

Maulizo ya uchunguzi

----

1. Ni malipizi gain Mungu aliwapa waisreli wenye hawakuamini kwamaba atawaongoza salama kuingia katika inchi aliyowaahidia?
   Aliwazunguusha katika jangwa muda wa miaka 40 mupaka wote walipo kufa.
2. Ni jina gain la sasa inchi ile ya ahadi inaitwa?
   ISRAELI
3. Taja wafalme kwanza wa Israeli:
   Mufalme Sauli, mufalme Daudi, mufalme Solomoni.
4. Ni wanani waliotumwa na Mungu kwenda kuwaonya wisraeli wakati walipomuasi Mungu ?
   Manabii.
5. Nani alikuwa nabi iwa mwisho?
   Yohana mubatizaji.
6. Ni nani unfikiri kuwa mukombozi aliyeahidiwa?
   Yesu Kristo.

SOMO LA 23

MWANA KONDOO WA MUNGU

Shauri kwa mwalimu

Hili ni somo la matudilio kuhusu sadaka ya munyama yenye Mungu alitoka kufunika zambi za watu wakati wa agano la kale. Itahakikisha kwamba wanafunzi wanaelewa sawasawa kama hii ilikuwa njia ya mupito tu mupaka pale mukombozi atakapokuja.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mambo ya walawi 1:1-3
Yohana 1:19-31
Waebrania 101-10
Mambo ya walawi 1:10
Waebrania 9: 11-14
1Petro 1:18-21.

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanfunzi

Uwafundishe wanfunzi sehemu hii

- Siku moja wakati yohana Mubatizaji alikuwa akibatiza watu katika mutoniYordani, aliona mutu anakuja kwake. Yohana alitamka maneno ya ajabu…,
- Alisema “tazama mwanakondoo wa Mungu anayekuja kuondoa zambi za ulimwengu”
- Ni nani huyu mwenye yohana anazungumzia na altaka kujulisha nini kwa maneno hayo?
- Kumbuka muda murefu uliopita kasha Adamu na eva kusikiliza maneno ya uongo ya shetani, Mungu alifukuza watoke bustani ya edeni kwa sababu ya vile waikataa kutii Mungu.
- Watu wote waliozaliwa kiisha Adamu na Eva walizaliwa wakiwa nwenye zambi na vile watatengananishwa na Mungu ikiwa ni pamoja na sisi; tunatawaliwa na Shetani.
- Mungu ni mtakatifu na mutakatifu na hivyo anajitenga na zambi zote.
- Mungu lazima alzihukumu zambi zote kwa njia ya kifo.
- Kwa sababu ua upendo mukubwa wa Mungu na huruma yake, aliyeahidia kama ataleta mukombozi ambaye ataziharibu nguvu za shetani juu ya watu, yeye atachukuwa hukumu ya zambi zao na kuwatengenezea njia ya kurudia katika jamaa ya Mungu.
- Mupaka hapo mukombozi atakapokuja katika dunia, Mungu aliwapatia watu njia ya mapito ya kumwendea yeye kurudi zambi zao ziweze kuondolewa.
- Njia jiyo ya mapito ni yenye ilionyesha kama waisraeli walitakiwa kutoa sadaka ya munyama dume bila kilema, kama vile mwanakondoo au mbuzi kwa kumuchinja na kuachilia damu yake itoke inje na kiisha kutoa mwili wa munyama huyo kama sadaka kwa Mungu.
- Ikiwa mutu atakubali mbele ya Mungu kama yeye ni mukosefu na kuhakikisha kama kwa sababu ya zambi zake alistahili malipizi ya kifo, na akikuja kwa Mungu alikubali kifo cha munyama huyo kuwa njia ya kufunika zambi zao.

- Abeli alikuja kwa Mungu kwa njia hii na Noa, na Abrahamu, Isaki, Yakobo, Musa, mufalme Daudi na wengine.
- Wakati Mungu anamupa Musa amri katika jangwa, Mugu aliamurisha kama ni lazima kuhani mkuu amwangie matoni ya damu ya mwanakondoo dume katikati ya sanamu mbili za malaika ndani ya hema.
- Damu ya mwanakondoo ilikubaliwa na Mungu kama njia ya kufunika zambi za waisraeli kwa mwaka mumoja. Kuhani mkuu alitakiwa kufanya hivyo mwaka kwa mwaka.
- Sasa ni kwa sababu gain Yohana mubatizaji anasema kama hapa kuna mutu mwenye atachukuwa zambi za watu wa dunia.
- Katika somo itafuata hiyi, tutajifunza mambo mengi yanayomuelekea mutu huyu na tutajua ni sababu gain yohana alimuita" Mwanakondoo wa Mungu".

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Yohana 1:29.

Maulizo ya uchunguzi

---

1. Ni maneno gain ya ajabu aliyoyasema Yohana Mubatizaji?
   "*Huyu ndiye mwanakondoo wa Mungu anayeondoa zambi za watu wa dunia"*
2. Kwa nini watu wametengwa na Mungu?
   Kwa sababu wote tumezaliwa tuko wenye zambi.
3. Ni namna gain Mungu anazihukumu zambi?
   Kwa kifo.
4. Ni nani ambaye Mungu aliahidi kumuleta katika dunia kuchukua malipizi ya zambi zetu ?
   Mukombozi Yesu Kristo.
5. Ni munyama wa namna gani mwenye kuhani mkuu alitakiwa kutoa sadaka ?
   Munyama dume asiye na doa.
6. ukimwuua munyama na ukamutoa sadaka kwa Mungu unafikiri kama Mungu atafurahiwa kwa na wewe na kukusamehe zambi zako ? *Hapana*.

SOMO LA 24

YESU NI NANI ?

Shauri kwa mwalimu

Uwakumbushe wanafunzi kama kuna Mungu mumoja ambaye yuko katika nafsi tatu zote zikiwa ni Mungu nafsi hizi hizi ni Mungu Baba na Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Yesu alizliwa kama mutu, lakini yeye ni Mungu.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mambo ya walawi 1 :10
Matayo 1 :18-25
Waebrania 4 :15
Isaya 7:4
2 Korintho : 5:21
1 Yohana: 3:5
1Petro: 2:22

Rudia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi.

Uwafundishe wanfunzi sehemu hii:

- Wanyama wenye Mungu aliwakubali kuwa sadaka wakati wa Agano la Kale walipaswa kuwa bila kilema ngambo zote.
- Walitakiwa wasiwe wagonjwa, wala wasiwe na kidonda chochote katika miiki yao, wasiwe vipofu, wala kuwa na ulema wa namna yoyote katika mwili.
- Ikiwa Mkombozi alieandaliwaa anakuja kuchukua zambi za watu wote wa dunia, ni lazima basi awe yeye naye bila kilema.
- Hii haitaki kusema kama I lazima asiwe na kidonda, asiwe mungnjwa. Kuwa Mutakaifu. Kuwa mukamlifu inataka kusema kama anatakiwa asiwe na zambi yoyote.
- Namna gani mwandamu azaliwe bila zambi?
- Adamu ni baba wa kwanza wa watu wote wa dunia, na kwa sababu ya zambi ya Adamu, watu wote wanzaliwa wakiwa ni wenye zambi.
- Mukombozi huyu alitakiwa azaliwe kwa namna ya pekee, il asiwe mwenye zambi yoyote.
- Hakuna neno haliwezekane kwa Mungu.
- Alimuchagua binti mudogo aliyeitwa Mariamu awe mama wa Mukombozi.
- Mariamu aliukuwa amechumbiwa tayari na mwanaume aliyeitwa Yosefu.
- Lakini mle ya wao kuoana, Mariamu akaonekana ana mamba!
- Ilitendeka neon la ajabu; Mungu Roho Mtakatifu alimutia Mariamu mutoto ndani ya tumbo lake.
- Mutoto huyo alikuwa Mungu Mwana alishuka kutoka mbinguni na kufanyika mwanadamu, aweze kuwakomboa watu na hukumu ya zambi.
- Mutoto huyu wa namna ya pekee alikuwa na majina mengi, jina lake moja lilikuwa Immanueli maana yake “Mungu pamoja nasi”.
- Jina lake lingine aliitwa… unaweza kupima? Ndiyo. Aliitwa yesu, maana yake Mwokozi au Mkombozi!.

- Yesu hakutoka kwa Adamu kama sisi, alitoka kwa Mungu, yeye ni Mungu; hivyoalizaliwa bila zambi.
- Yesu alikuwa mwanadamu na tena Mungu. Mungu amekuja ndani ya mwili wa mwanadamu kuishi pamoja na watu duniani.
- Mungu aliona vizuri yesu awe na baba wa duniani wa kumulea, hivyo Malaika alimwambia Yesefu amukubali Mariamu kuwa muke wake hata kama anaonekana ana mamba.
- Hivyo, usiku mumoja katika muji wa bethelehem, katika inchi ya Israeli, yesu alizaliwa kama vile manabii walivyo kuwa walikwisha kutabiri miaka mingi iliyopita.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Matayo 1:23.

Maulizo ya uchunguzi

----

1. Wanyama waliotolewa sadaka kwa Mungu walitakiwa kuwa wakamilifu, kukamlika huku kunataka kusema nini?
   Wasiwe wagnjwa wala wasiwe na vidanda wasiwe vipofu wala vilema.
2. Kwa nini Mungu alitoa ahadi ya kuleta Mukombozi?
   Aje kuchukuwa zambi za watu wa dunia.
3. Mukombozi alitakiwa kuwa mukamilifu yeye naye, mana yake nini? *Alitakiwa kuzaliwa bila zambi.*
4. Mariamu alipata mamba namana gain?
   Mungu Roho Mutakatifu alitia mutoto ndani ya tumbo la Mariamu.
5. Jina Immanueli maana yake nini ?
   Mungu pamoja nasi
6. Je yesu ni Mungu?
   Ndiyo, Yesu ni Mungu.

SOMO LA 25.

YESU ANAKOMAA

Utangulizi kwa Mwalimu

Yesu ni Mungu lakini tena ni Mwandamu. Alikomala kama watoto wengine, ila yeye hata mara moja hakukosa kumuheshimu Baba.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Luka 2 :8-20 Matayo 2 :1-2.

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi.

Fundisha wanafunzi nafasi hizi.

- Ule usiku ambao Yesu alizaliwa, Mungu aliwatuma malaika kuambiya wachungaji habari njema kama mukombozi wa dunia amezaliwa.
- Wachungaji hao walikuwa inje ya muji wa Bethelehemu wakichunga kondoo zao
- Gafula wamalaika wengi wakatokea juu wakiimba, wakisifu Mungu kwa Makubwa hayo yaliyotokeya.
- Wachungaji waliacha kondoo zao wakaenda mujini kumutafuta mutoto aliye zaliwa.
- Huko, walikuta mariamu na Yusefu na Mtoto Yesu akiwa ndani ya Hori ya ng'ombo, wakapiga magoti na kumwabudu motto aliye zaliwa.
- Kiisha walimuambiya yeyote waliye kutana naye maneno yenye malaika wamewaambiya kuhusu Yesu.
- Yesu ndiye Mukombozi aliyeahidiwa yule mwenye Mungu alisema kama atakuja kuwakombowa watu kutokz katika hukumu ya zambi zao.
- Yesu aliwapata wengine wengi wakati alikuwa motto.
- Mungu alitiya nyota nzuri wakati Yesu alizaliwa.
- Watu wa kutoka inchi za mbali walifatilia ili nyota mpaka kwenye Yesu alizaliwa.
- Hao watu walitleta matabishi na wakamwabudu yesu sababu walimujuwa kuwa ni mutu Bora na wa kipekee, yesu ni Mungu Mwana, ni mufalme wa wafalme na Mukombozi wa wale wanao muamini yeye.
- Kadiri ya ginsi Yesu alivyoendeleha kukomala, Mungu alimuongoza na kumilinda katika kitu chote. Alifikiri, akaongeya na kufanya.
- Yesu aliheshimu kila sheria ya Mungu.
- Hakufanya zambi hata mar moja kama ginsi sisi tunavyofanya, sababu hukuzaliwa akiwa mwenye zambi kama sisi.
- Sisi tulitokeya kwa Adamu, ila yesu alitokea kwa Mungu.
- Yesu alikomala a kuwa mutu muzima mwenye akili, akimpendeza Mungu Baba na wanadamu.

Vesi za kukumbuka za kuwafundisha wanafunzi kwa mupango kiisha somo.

Luka 2:52.

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Ni wanani wliyotumwa na Mungu kwa wachungaji kuwapasha habari ya kama Mukombozi alizaliwa?
   Malaika
2. Je, Yesu alizaliwa munyumba ya muzuri?
   Hapana, alizaliwa katika hori ya ng'ombe.
3. Ni kitu gain chenye Mungu aliweka juu kuwaongoza wale watu mpaka kwenye Yesu alizaliwa?
   Nyota
4. Je, Yesu alikosa kumuheshimu Mungu Baba hata mara moja? *Hapana*
5. Kwa nini hatumutii Mungu ?
   Kwa sababu tumetokeya kwa Adamu piya tumezaliwa kuto wenye zambi.
6. Je Yesu naye alitoka kwa Adamu?
   Hapana, alitoka kwa Mungu.

SOMO YA 26.

ZAWADI ILIYOKUBWA KWA WATU WOTE.

Shauri kwa Mwalimu

Kwa kuhifanya somo hiyi ipendeze, unaweza kuwa patiya wanafunzi zawadi kidogo, kama mbombo au keke wakule pamoja; somo hili linahusu Yesu aliye zawadi kubwa kuliko zote (somo hili linaweza kufundishiwa piya siku ya Noeli).

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Yohana 6: 40
Matendo ya Mitume 2:22-23.
1 Yohana 4:9-10.
Yohana 20:30-31
Waefeso 2: 8-9
Ufunuo 22:17.

Rudiya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Fundisha wanafunzi na fasi hizi:

- Siku ya kuzaliwa maana yake nini? Siku ya kuzaliwa ni siku yenye wewe ulizliwa.
- Kama ulialiwa tarehe 10 julai, 1994, basi kila mwaka inafika tarehe hizo utafanya kukumbuka siku yako ya kuzaliwa.
- Katika mita zimoja zimoja, watu wanatoaka matabishi wakati wa sikuu ya kuzaliwa, au wanakula chakula kizuri sana wakiwa katika kusherekeha.
- Yesu naye ana siku yake ya kuzaliwa.
- Je kuna umoja wenu anaye juwa siku ya kuzliwa kwa Yesu?
- Ndiyo ni ni tarehe 25.12
- Siku hiyo tunaita Noeli
- Mungu alitutupatiya zawadi iliyo kubwa siku ya Noeli
- Siku hiyo alitupatiya yesu.
- Yesu,Mungu wana alikuja duniani miaka 2000 iliyopita tokea siku hiyi.
- Alikuja kama motto kidogo, aliyezaliwa na Mariamu katika inchi ya Israeli.alikomala na kufanya maishara menggi yenye uwezo, kama kuwaponya vipofu wakaona tena, kufufuwa wafu kufukuza pepo wabaya na maishara zingie nyingi
- Aliyafanya maishara hayo yote kuonyesha kwamba yeye ni Mungu Mwana aliye tumwa kutoka mbinguni.
- Watu wamoja hawakumuamaini na wakamuhuwa kwa kumupigiliya misumari musalabani.
- Huyu ndiyo ulikuwa mpango wa Maungu kwa Yesu, kwa sababu Yesu alikuja duniani ili atoe maisha yake kwa ajili yetu sote.
- Ukumbuke kwamba Mungu ni Mutakatifu na mukamilifu na kwamba ni sherti ahukumuzambi (kifo)

- Mungu alimuhukumu Yesu kwa sababu ya zambizetu,sababu wote wenye wataamini kupitiya yeyey watasamehewa zambi zao na kuwaweka huru kutoka utumwa wa shetani na kufanywa wana wa Mungu.
- Ni zawadi gain iliyo muzuri kupita hiyi yenye tulipewa siku ya Noeli!

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Yohana 3:16.

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Siku ya kuzaliwa maana yake nini?
   Ni siku ambayo kila mwaka unakumbuka tarehe na mwezi uliyozaliwa.
2. Ni siku gain yenye tunakumbuka kuzaliwa kwa yesu?
   25 december ndiyo inayo itwa Noeli
3. Sababu gani yesu alifanya maishara hapa duniani?
   Ni sababu atuonyeshe kwamba ni mungu mwana aliyetoka mbinguni.
4. Je kila mutu alimuamini kwamba yeye ni Mungu Mwana? Hapana
5. Sababu gani ilimupasa Yesu kufa ?
   Sababu abebe hukumu ya zambi zetu
6. Ni kwa namna gani unaweza kusamehewa zambi zako ?
   Ni kwa kumuamini Yesu aliye kulipia zambi zako kwa kukuta msalabani.

SOMO LA 27

ROHO MUTAKATIFU NI NANI

Shauri kwa Mwalimu.

Katika somo hili tunamuonyesha Roho Mutakatifu mu wakati wa Agano la Kale, Mungu aliwapatiya nguvu na mamlaka watu wachache ; kwa ajili Roho mutakatifu. Wakati huu wa Agano jipya, Roho Mutakatifu anahikala ndani ya wote wenye kumuamini Yesu kama mwokozi wao.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mwanzo 1 :1-2
1 Samweli 16 :13
Luka 3:21-23
Yohana 14:15-18
Matendo ya Mitume 10:37-38.
Kutoka 35 :30-35
Zaburi 51 :11
Yohana 7:37-38
Matendo Mtume 1:4-5.

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanfunzi.

Fundisha wanfunzi nafasi hiyi.

- Kumbuka kwamba piko Mungu umoja tu wa kweli aliye mzima.
- Yuko katika nfsi 3 nazo zote ni Mungu wa kilingana
- Piko Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu roho Mtakatifu.
- Mu wakati wa agano la Kale,yaani mbele yesu, Mungu Mwana Kuzaliwa duniani, Mungu Roho Mutakatifu aliwapatiya nguvu watu wamoja kwa kuwasaidiya kufanya vitu Bora vyenye Mungu alitaka wafanye.
- Roho Mutakatifu alimusaidiya Nuhu kumutii na kuwashauri watu kuhusu garika.
- Roho mutakatifu alimusaidiya Ibrahimu, Isaka na Yakobo kumutii Mungu
- Roho mutakatifu alisaidia Musa kuandika chini maneno ya Mungu nayo ndiyo yako sasa katika biblia.
- Vitabu vitano vya kwanza mu biblia viliandikwa na Musa
- Roho mutakatifu alimusaidiya mufalme Daudi kuwa mufalme bora na akaandika Mambo mengi katika Zaburi yenye yapo sasa katika biblia yetu.
- Roho mutakatifu alimupa Mariamu mutot na tena Roho mutakatifu alimusaidiya Yohana Mubatizaji kufanya kazi zake kwa ajili ya Mungu.
- Roho mutakatifu aliwapatiya uwezo watu hao wote na wengine kufnaya kazi bora za Mungu.
- Roho mutakatifu piya alimusaidiya Yesu kwa wakati wenye alikuwa anahishi hapa duniani kama mwanadamu.

- Yesu alikuwa na miaka karibu 30 wakati wenye alibatizwa na nabii Yohana mubatizaji.
- Yesu wakati alitoka mu maji alikuwa tayari kujazwa roho mutakatifu, kusdi aweze kutenda kazi zenye Mungu amepngiliya.
- Japo hiyo, Yesu ni Mungu, wakati wenye aliishi hapa duniani kama mwandamu aliomba kumtegemea Roho mutakatifu kusudi apate nguvu za kufanya kazi ya Mungu hapa duniani.
- Roho mutakatifu aliongoza kila kituchenye Yesu aliwaza kusema na kufanya wakati aliyo kuwa hapa duniani.
- Leo hiyi, Roho mutakatifu ndiye anawasaidiya watu wengi wenye kuamuamini yesu kuwa mwokozi wao.
- Kiisha mu somo za kufuata, tutajifunza mengi ya kuhusu kazi za Roho mutakatifu na namna gani anaweza kukusadiya ili uwe mtumwenye Mungu anapenda.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

1 Wakorinto 3 :16.

Maulizo ya uchunguzi

1. je piko Mungu umoja au miungu watatu ?
   Mungu ni umoja tu
2. Ni nani alimusaidiya Musa kuandika maneno ya Mungu ?
   Mungu roho mutakatifu.
3. Ni nani alimusaidiya mufalme daudi kuwa mufalme Bora ?
   Roho mutakatifu.
4. Ni nani anayewasaidiya wale wanao muamini Yesu leo ?
   Roho mutakatifu.
5. roho mutakatifu ni nani ?
   Ni Mungu.

SOMO LA 28.

YESU ANAJARIBIWA NA SHETANI

Shauri kwa mwalimi.

Somo hili linaonyesha kama watu wale wanao mwamini Yesu wanaweza kumutii Mungu. Yesu yeye hakujitowa kwa shetani kama Adamu na Eva. Kwa hiyo, Mungu anaweza kuwasaidiya wamutii wakati wanapokutana na na jaribu kama wakimwomba.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Matayo 4 :1-11
Yohana 10 :14-18
Waebrania 1 :12-15
1 Yohana 5:19.
Yohana 8 : 44
1 Wakorinto 10 :13
Waebrania 4 :15-16

Funshisha wanafunzi nafasi hiyi

- Kwanza turudiye ku mwanzo wa Biblia. Unakumbuka jinsi shetani alivyo shawishi Adamu na Eva mpaka wakakosa kutii mapenzi ya Mungu?
- Adamu na Eva walikubali kusikiya uongo wa shetani kuliko kumutii Mungu
- Na kwa sababu ya kukosa utii kwao hawakukuwa tena watoto wa Mungu walikuwa chini ya utawala wa shetani.
- Sisi sote tumetokeya kwa Adamu na tumezaliwa chini ya utawala wa shetani.
- Wakati yesu alipokuwa akishi duniani Shetani alijaribu kumfanya Yesu awe chini ya mamlaka yake.
- Shetani alitaka yesu naye amukosee Mungu Baba, kusudi asionekane kwamba ahana zambi tena na ni mutkamilifu
- Shetani hakutaka Yesu awe Mukombozi aliahidiwa kwamba ata zivunja nguvu na utawala wa shetani.
- Kiisha Yesu kubatizwa, Roho mtakatifu alimwongoza kwenda mujangwa na huko yesu alifunga siku 40 muchana na usiku.
- Shetani alikuja kusudi apate kumujaribiya.
- Yesu alikuwa ameisha sumbuliwa na njala, japo hiyo hakumutii Shetani
- Shetani alipima tena kumujabiya Yesu ili asimuheshimiye Mungu Baba lakini Yesu hata mara moja hakufanya zambi.
- Alimutii Mungu kila saa na kwa namna zote.
- Kwa sababu Yesu hakumutii shetani hata mara moja, anaweza kuwasaidiya wale wote wanaomuamini kuwa Mwokozi wao wakati wanapojaribiwa na shetani.
- Shetani anakosa wakati mutu anapohamuwa kumufuata Yesu kwa hiyo atakufanya na weye usimuheshiye Mungu piya.

- Usisikilize uongo wa shetani yeye anapenda mamabo mabaya yatokeye kwako.
- Shetani ni muhuaji na ni baba wa uongo. Kuwa huwa na kuwaharibu watu wote.
- Kama marafiki wako wanataka kuiba kitu fulani, wewe ukatae kwenda nao, uwaachiliye waende peke yao.
- Kama unajaribiwa kusema neno baya kwa rafiki yako, ufanye mdomo wako ili usisemi chochote.
- Ukumbuke kwamba yesu anajuwa majaribu yako kwani naye hata yeyey alijaribiwa kama sisi.
- Wakati ambao utakapojaribiwa kufanya mambo mabaya umuombe Mungu ili akusaidiye kusema « hapana » naye ni mwaminifu na atakusaidiya.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Waebrania 2 :18.

<u>Maulizo ya uchunguzi.</u>

1. Wakati wenye Adamu na Eva wamemukosea Mungu ni nani aliyekuwa akiongoza nyuma ya hapo ?
   Shetani
2. Ni kwa sababu gani shetani alitaka Yesu amutii ?
   Kusudi Yesu asionekane hana zambi piya asikuwe mukombozi aliye haidi.
3. Je, Yesu alimutii shetani hata mara moja ?
   Hapana, hata kidogo.
4. Je shetani anatujaribiya hata sisi tusimutii Mungu ?
   Ndiyo.
5. Ni kwa nini Shetani anatujaribiya kufanya mambo mabaya ?
   Ni kwa sababu angali anataka kuendeleya kutawala.
6. Ni nani anaweza kutusaidiya kukatala mipango ya shetani ?
   Yesu.

SOMO LA 29.

YESU ANAWALISHA WATU 5000

Shauri kwa Mwalimu.

Watu waliyo amini Yesu waliamin kwasababu mbalmbali. Hata sisi, tunaombwa kuamuwa kama tutaamini kwamba Yesu ni mukombozi wa Dunia. Tunakuwa na Biblia ambayo inatusaidiya kufanya uamuzi.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Matayo 4 :23-25
Yohana 1 :45
Yohana 5 :46
Yohana 20:30-31.
Matayo 7 :27-29
Yohana 4 : 39-42
yohana 6 :1-14.

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanfunzi.

Fundisha wanfunzi nafasi hii.

_

- Yesu alikuwa na umri wa miaka 30 kwa kipindi hiki
- Alikuwa aliishajazwa na nguvu za Roho mutkatifu, na akaanza kazi yake yenye Mungu baba alimupa ahifanye kwa wakati wote alipokuwa duniani kama mwanadamu.
- Yesu alitumiya wakati mwingi kutembeleya muji huyu na kwenda mu muji ungine mu inchi ya Israeli.
- Watu wengi walimufuata na kumusikiliza Yesu wakati wa kuonge kwake kwani aliongeya kwa mamlaka apana kama mwalimu wao wa dini.
- Yesu alitafsiri maandiko mtakatifu mu agano la kale yenye Musa na manabii wengine walipewa na Mungu kwa miaka mingi iliyopita
- Yesu alijuwa kwa ukweli maana ya yale maandiko matakatifu kwani yeye alikuwa Mung Mwana na hayo maandiko yalisema kuhusu yeye.
- Watu wengi walikubari kwamba ni yeye Mukombozi mwenye aliahidiwa yule aliye aliyeahidiwa Adamu na Eva, Nuhu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo na wengine.
- Waliamii kwamba ni Yesu atawaokoa watu mikononi mwa shetani, zambi na mauti.
- Kwa ajili ya imaniyao ndani ya Yesu Mungu aliwahitika kuwa watoto wake.

- Yesu aliwachaguwa wanaume 12 akawafanya kuwa wanfunzi wake, na wajifunze kwake na wafanye kazi pamoja naye, alipokuwa akitembea, akifundisha, akiponesha magonjwa na akihubiri.
- Watu wengine walianza kumwamini Yesu kwa sababu waliona anafanya maishara mingi yenye nguvu.
- Watu hawa hawakujulikana kama wanfunzi wake
- Wakati moja yesu alipokuwa akiwafundisha wanfunzi wake, kundi kubwa ya watu walikusanyika ili wamusikilize akifundisha.
- Yesu aliwaambiya wanafunzi wake wawapatiye chakula, kwani saa zilikuwa zimeisha pita sana watu wakiwa na njala.
- Kulikuwa watu wakupita 5000! Wangepata chakula wapi cha kuwaenea watu hawa wote?
- Chakula walikuwa nacho ilikuwa mikate kidogo tano na samaki kidogo mbili.
- Yesu alijuwa hayo! Alikuwa na mpango muzuri sana.
- Yesu alikamata vyakula vile, akamushukuru Mungu aba akawapatiya wanafunzi wake wagabuliye watu wale.
- Je uanweza kukumbuka ni kitu gain chenye kilifanyika?
- Ndiyo, chakula kilikuwa kikiongezeka sana kama vile walivyo kigabua. Kikawatosha watu wote, kila mutu sawa sawa na mahitaji yake a kukabakiya vikapu 12 vya vyakula.
- Ni ishara ubwa gain hii! Watu wengi wakaanza kumwamini Yesu kiisha kuona mambo yenye alifanya.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Yohana 6:14.

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Kwa nini Yesu aliweza kuyajuwa maandiko mataktifu vizuri sana? *Kwa sababu yeye ni Mungu Mwana, na maandiko matakatifu yana sema mambo kuhusu yeye.*
2. Marafiki 12 wa Yesu waliwaita aje? *Wanafunzi wake.*
3. Ni watu wangapi walikulishwa chakula? *Zaidi ya watu 5000.*
4. Kitu gain kilitokea kiisha Yesu kushukuru kwa ajili ya chakula? *Kilikuwa kikiongezeka sana kama vile wanafunzi walivyo kigabula.*
5. Ni vikapo ngapi vya vyakula vyenye vilibakiya kiisha watu kutosheka? *Vikapu 12.*

SOMO LA 30.

YESU ANASAMEHE MTU ZAMBI.

Shauri kwa Mwalimu.

Mu makanisa zimoja wanfundisha kama wachungaji na wasimamizi wanaweza kuwasamehe watu zambi zao, wanahakikishiyawafuasi wao kwamba zambi zao zimeisha samehewa wanapokuwa na wasiwasi. Lakini tujuwe ni Mungu peke aliye na uwezo wa kusamehe zamb, wakati tuna tunapo tubu zambi zetu kwake.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Marko 2:1-12 Yohana 1:6-11
Yohana 20:30-31. 1Yohana 1:9.
1 Yohana 2:1-2.

Rudiliya maulizo ya somo lililopita pamoja na wanfunzi.

Fundisha wanfunzi nafasi hii.

- Watu wengi walifuata Yesu na wanfunzi wake kote pale kwenye walihenda.
- Wengine walikuja kusikiliza mafundisho, wengine mufano walimu, walimu wa sheria walikuja kwa lengo la kumusikiya Yesu kama atasema mambo mabaya, wengine walikuja walikuja kwa sababu walizani kama yesu takuwa mufalme waon a wengine walikuja kwa sababu walikuwa wagonjwa hata wakahitaji yesu awaponye.
- Wakati moja Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakifundisha ndani ya nyumba ili yala watu ikayala sana hata hapakuwa na fasi tena ya mtu kuingiya kwa kupita ku mulango.
- Watu ine walikuja kumutazma yesu nao wanamubeba ndugu yao aliye kuwa mugonjwa; akiwa kwenye kitanda chake.
- Mutu huyu alikuwa hawezi kitingiza migulu yake ao kutembeya kabisa.
- Ndugu zake walikuwa na imani kama Yesu ataweza kumuponyesha wakifika tu karibu naye.
- Wakapata wazo.

- Wakapanda juu ya dari ya nyumba wakatibowa tundu kwa kushukiya pale kwenye Yesu alikuwa anfundisha.
- Wakamutelemusha mugonjwa yule akiwa kwenye kitanda chake kwa kupitiya lili tundu hata karibu ya yesu.
- Yesu akaona kwamba wale watu wakiwa na imani kwake hata akapendezwa na imani yao kwake.
- Yesu akamuambiya yule mugonjwa, Mwanangu, zambi zako zimesamehewa.
- Wamoja mu walimu wa sheriya wenye walikuwa pale walisikiya jinsi yesu alivyo sema hayo.
- Wakaana kuwaza, sababu gain mutu kawaida anaweza kusameya zambi ni Mungu tu ndiye nao uwezo wa kasameya zambi.
- Hawakuamini kama Yesu ni Mungu katika mwili, nay eye na mungu Baba ni kitu kimoja, na kwa sababu hiyo anao uwezo wa kumusameya mutu zambi.
- Yesu alijuwa yale walikuwa wanawaza sababu Mungu anajuwa kila kitu
- Kwa kuwaakikishiya watu wale kama yeye ni Mungu, Yesu aliponya migulu ya yule mutu na akamuamabiya kamata kitanda chako uhende nyumbani.
- Kila mutu aliye hona ishara hiyo alimusifu Mungu na watu wengi wakaanza kuamaini kwamba ni kweli Yesu ndiye Mukombozi aliyeahidiwa.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Marko 2:7 (sehemu ya mwisho)

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Sababu gain walimutafuta popote alipokuwa akienda?
   Wengine kumsikiliza akifundisha, wengine kumusikiya akisema wala labda akitenda mambo mabaya NK.
2. Ni mahali gain Yesu alikuwa akifundisha na watu 4 wakamuleta ndugu yao aliye kuwa mugonjwa? Ndani ya nyumba.
3. Sababu gain walimuleta mugonjwa yule kwa Yesu? Walikuwa na imani kwamba yesu anaweza kumuponya.
4. Ni neon ganai la kwanzalenye yesu alimuambiya yule kijana? Mwanangu, zambi zako zimzsamehewa.
5. Ni nani anaye weza kusamehe zambi peke yake ? Mungu.
6. Je Yesu ni Mungu ? Ndiyo ni Mungu na alihonekana kama yeye ni Mungu kwa kuponesha migulu ya yule mugojwa.

SOMO LA 31

UNASTAHILI KUZALIWA MARA YA PILI

Shauri Kwa Mwalimu

Watu mingi wanaamini kuwa, wanaweza kumupendeza Mungu kwa kufanya mambo mazuri. Hii siyo kweli watu wote wanazaliwa na zambi na ni sharti wahukumiwe kwa ajili ya zambi zao kwenda kanisani na kufanya matendo ya haki, havitafanya Mungu atukubali. Kuwa na imani kwa yesu kunatufanya kuwa wenye haki kwa Mungu.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Yohana 3 :1-18 1 Samweli 16 :

Rudilia Maulizo Ya Somo Lilipita Pamoja Na Wanafunzi.

Uwafundishe Wanafunzi Fasi Hii :

- Katika somo la 26 tulisema kuhusu siku ya kuzaliwa, munakumbuka nini ? je, munajuwa kwamba inawezekana kuwa na siku mbili za kuzaliwa ?
- Musikiye hadisi hiyi na mutajuwa.
- Siku moja mutu aliyeitwa nikodemu alianda kumuona yesu.
- Alikuwa ni mutu muhimu sana katika Israeli, alikuwa muyuda na mufarisayo.
- Hii inamaana kwamba alitoka katika jamaa ya Abrahamu na pia alikuwa wa sheria.

- Nikdemu alifanya nguvu kutii sheria zote ambazo Mungu limupa musa.
- Alitunga hata pia sheria mupya ambazo watu waliombwa kuzitii.
- Alikuwa anaongea muda murefu, akiomba kwa sauti kubwa katika kanisa, alikuwa anatoa sehemu moja ya kumi kwa kila kitu alichopata. Hiyo inaitwa sehemu ya kumi.
- Alikuwa anafunga kula chakula ili ajaribu kumupendeza Mungu.
- Alikuwa anavaa manguo ya muzuri ya kufanana hata kila fasi alikuwa akipita watu wote walizania kwamba yeye ni mutu wa maana saana tena wa ajabu kwa Mungu.
- Nikodemu alifurahi sana na hali yake na akazania kwamba hata Mungu ananmupenda.
- Yesu alimupenda nikomu na alijuwa kila kitu kuhusu maisha yake.
- Mungu anajuwa kila kitu kuhusu sisi wote na antupenda pia.
- Yesu akamwambia nikidemu kwa upole kwamba kufata na na haya yote ”kuzaliwa mara ya pili”.
- Nikodemu hakuelewa. Ni jinsi gani ataweza kurudia ndani ya tumbo la mama yake na kuzaliwa mara ya pili na yeye tayari ni mutu mukubwa? Siyo hivyo yesu alitaka kusema.
- Yesu alimueleza kwamba watu wote pamoja na nikodemu wamezaliwa na wakiwa wanatengena na Mungu kufuatana na kutokutii kwa Adamu.
- Watu wote wanapatikana katika familia ya shetani na hawawezi kujigomboa na hukumu ijapokuwa wana fanya matendo mazuri ya kmufurahisha Mungu.
- Ni Mungu peke ndiye anaweza kutuokoa kutoka katika hukumu ya zambi zetu.
- Ni kwa kuamini katika yesu tu, ndipo tunawezakuokolewa na kuzaliwa mara ya pili katika familia ya Mungu na siku moja tutaishi mbinguni na Mungu milele na milele.
- Roho zetu zinazaliwa upya hutoka katika familia ya shetani na kuingia katika familia ya Mungu.
- Hii ndiyo maana ninawezakuwana siku mbili za kuzaliwa! Moja, tulipozaliwa kutoka katika tumbo za mama zetu, na ya pili tunapochagua kuamini yesu na kuwa watotowa Mungu.
- Mpaka sasa uko na siku ngapi za kuzaliwa?

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Yoana 3:3

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>:

1. Je, yesu alimupenda nikodemu ? ndiyo Mungu anapenda kila mutu.
2. nikodemu alifanya vitu gani ili amupendeze Mungu? Kutii sheria zote, kufunga kula chakula, kuomba na kutoa pesa .k.
3. je, haya ni mambo ya muzuri kama vile nikodemu alikuwa akifanya? Ndiyo

4. je, Mungu alimukubali nikodemu kama mutoto kwa kufanya mambo hayo? Hapana hakumukubali.
5. sababu gani Mungu hakumkubali nikodemu kama mutoto wake?
6. kwa sababu Mungu hawezi kutukubali kuwa watoto wake, mupaka zaliwa mara ya pili.
7. tunaweza kuzaliwa mara ya pili namuna gani?
8. kwa kuamini yesu kuwa bwana na mwokozi wetu.

SOMO LA 32.

MBINGUNI AO JEHANAMU?

Shauri Kwa Mwalimu:

Biblia inafundisha kwa uwazi kuwa kisa kifo ni hukumu, na kisha hapo tunapelekwa mbinguni ao jehanamu, itatokana na kama tulimwamini Mungu ao hapana. Hii sasa ndio wakati wa kuamuwa kuhusu yesu. Kisha kufa utakuwa tayari umechelewa.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Matayo 10:28
Luka 23:39-43
Yohana 14:1-3
1 Wakorintho 2:9
2 Wakorintho 5:1-8
Ufunuo 21:1-8
Luka 16:19-31
Yohana 3:36
Warumi 5:12
1 Wakorintho 15:35-58
Waebrania 9.

Rudilia Maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi:

- Biblia inatuambia kwamba hapo mwanzo Mungu aliumba dunia yenye kuenea.
- Hakukuwa na magonjwa, maumivu, mateso ao kifo, kila kitu kilikuwa muzuri.
- Mungu aliumba Adamu na Eva waishi, katika dunia iliyo kamili na wanageweza kuishi ndani milele na uwepo wa Mungu.
- Mungu aliwapenda saana, na aliwaonya kuhusu kutokutii haagizo yake.
- Matokeo ya kukosa kutii Mungu ni kutengwa na Mungu, kufa kimwili na mwisho kabisa kutupwa katika ziwa la moto.
- Adamu na eva walichaguwa kumusikiliza shetani na wakageuka agizo la Mungu.

- Na kutokana na kwamba watu wote walitoka kwa Adamu na Eva, hakuna atakayeishi milele duniani.
- Tumezaliwa tukiwa na zambi na miili yetu sherti itakufa.
- Lakini biblia inasema kwamba, miili yetu ni mahema ao nyumba cha muhimu ni roho zetu ambazo zinakaa ndani ya mili yetu.
- Roho zetu haziwezi kuishi hapa duniani bila miili yetu.
- Wakati miili yetu inapokufa (kufa kimwili) roho zetu zinaendelea kuishi milele.
- Kuna fasi mbili tu ambazo roho zetu zinaendelea kuishi.
- Roho za wale wanao amini kwamba yesu alikuja kufa ili kuchukuwa hukumu ya zambi zao, wataenda kuishi na Mungu milele, huko watapewa miili ya mupya, ambayo haitakufa tena.
- Roho za wale wasio amini ndani ya yesu zitatengwa na Mungu na kutupwa katika ziwa la moto.
- Wakati yesu alipokuwa anaishi hapa duniani, aliponya kila mugonjwa aliye kwenda kwake na alifufua wafu.
- Yesu alifanya hivyo ili kuwaonyesha watu kuwa yeye ni Mungu na kwamba Mungu ni mukubwa kuliko shetani magonjwa na kifo.
- Sisi sote tutakufa kimwili siku moja, ao kwa kuuguwa ao kwa kuzeheka n.k.
- Lakini kama unaamini katika yesu, usiogope kufa, sababu siyo mwisho, ndio sasa mwanzo!
- Biblia inatuambia kwamba Mungu anatutayarishia vitu vizuri sana huko mbinguni kwa wale wanaomupenda. Mambo ambayo hatuwahi kuona katika maisha yetu kusikia wala kufikiri.
- Ni matumaini gani ya muzuri ambayo watoto wa Mungu wakonayo kwa siku zinazokuja! Umushague yesu leo, mbele ya muda haujapita!

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Yohana 11:25 (sehemu ya mwisho).

Maulizo ya Uchunguzi

1. Ni sababu gani watu wote wanakufa*? Zambi na kifo vililetwa duniani kupita kwa Adamu hivo ni sherti tutakufa.*
2. je, roho zetu pia zitakufa? *Hapana zinaisha milele*
3. ni fasi gani roho zetu zinaweza kuishi ? *Mbinguni ao jehanamu*.
4. ni roho za watu gani zinaenda kuishi Mbinguni ? *za watu wanaokubali na kuamuni katika yesu.*
5. ni roho za watu gani zinaende kuishi jehanamu ? *za watu wasiokubali na kuamini katika yesu.*

6. je, wanao amini katika yesu wanaweza kuogopa kufa ? *hapana, sababu Mungu amewatayarishia makao muzuri Mbinguni.*

SOMO LA 33.

YESU ANAWEZA KUKUSAIDIA.

Shauri Kwa Mwalimu

Siku hizi watu wanaihi katika hali mugumu sana, kama vile umasikini, ulevi madawa ya kulewesha, magonvi, uvamizi wa ngono kwa nguvu. Shetani anawaruhusu watu kuchagaguwa kujinyonga kama njia ya kuachana na shida zao. Yesu anaweza kukusaidia kwa kumaliza shida yako, kwa sababu hakuna kisichowezekana kwa Mungu.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Isaya 41 :10-13
Marko 9 :14-27
Warumi 8 :35-39
Marko 5 :1-20
Yohana 8 :44
Matendo ya mitume 16 :16-3

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi.

Wafundishe wanafunzi fasi hii :

- katika somo iliyopita tulijifunza kuwa roho zetu haziwezi kuishi hapa dunia bila kuwa na miili yetu. Wakati tunapokufa, roho zetu zinakwenda ao mbinguni, au jehanamu.

- Kuko mila zingine nyingi ambazo shetani aliwadanganya watu kuamini kwamba mababu zao waliowatangulia hapo zamani na walikufa wanaendelea kuishi hapa duniani.
- Roho zinazoendelea kuishi hapa duniani kisha kufa ni mapepo wachafu bgaani wafuasi wa shetani.
- Wakati ingine mapepo hao wanaishi ndani ya watu na kuwaruhusu kufanya matendo mabaya.
- Lakini ukumbuke kwamba Mungu ni mukubwa kuliko shetani na anauwezo juu ya shetani na malaika zake.
- Yesu alionyesha uwezo huo wakati alipokutana na mutu aliyekuwa anaishi milimani huko Israeli.
- Mtu huyo alkuwa anaagonjwa na mapepo hao mubaya.
- Siku mujima. Mtu huyo alikuwa anapiga kelele na kujikatakata na vipande vya majiwe.
- Watu walipima kumufunga minyororo, lakini ampepo hao walimupatia nguvu ya kukata minyonyororo hiyo.
- Hakuna mutu aliyeweza kumusaidia sababu mutu huyo alikuwa chini ya uongozi wa mapepo.
- Wakati mutu huyo alipomwona yesu anakuja, mapepo ndani yake yalipiga kelele sababu walijuwa kwamba yesu ni Mungu mwana.
- Walijuwa kwamba yesu ikona uwezo juu yao na wakamuomba asiwapeleke katika ziwa la moto kama hukumu yao.
- Mungu iko na mpango wa kuhukumu shetani na malaika zake siku zinazokuja mbele, na mapepo hao walijuwa hivo, na ndipo walimuomba awapeleke kwa nguruwe ambao walikuwa karibu na fasi hiyo.
- Yesu aliwaruhusu mapepo hao kuingia ndani ya nguruwa na ndipo hawa nguruwe wakatumbukia wote ndani ya bahari na wakazama.
- Baada ya mapepo kumwacha yule mutu, alivaa manguo yake na akakaa chini akiwa kimya.
- Yesu akamwambia aende nyumbani na awaabie familia yake yale ambaya Mungu amemufanyia.
- Huyo mutu hakuwa na uwezo wa kujiokowa kutoka katika uongozi wa mapepo, yesu tu ndiye aliyemuweka huru.
- Hata leo shetani angali anawafanya watu wajiona kwamba hawawezi kuachana na matatizo ambayo wako nayo.
- Wanajiona kuwa hakuna anayeweza kuwasaidia.
- Hapo ndipo shetani anawaingia watu na kuwapa shauri kwamba ni sherti kufa kuliko kuishi katika mateso na matatizo.
- Sehemu ya watu wanasikilia uongo huo wa shetani na wanajiuwa.
- Usisubutu hata mara oja kufanya hivyo ! hii siyo jibu ya matatizo yako.
- Shetani anamuchukia Mungu na wanadamu, na anataka kuwaharibisha watu.
- Kila wakati kuko musaada kwa kila shida unalo kutanana nayo.

- Kwanza umwambie Mungu shida yako, na umwambie mutu unayemwaminia kama vile baba yako, mama yako, muchungaji wa kanisa mwalimu n.k

Ukumuke kwamba hakuna kisichowezekana kwa Mungu.

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Isaya 41:13

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. wakati tutakufa roho zetu zitaenda wapi? *Mbinguni ao jehanamu*
2. Ni Roho gani zinazoishi hapa duniani? *Roho za pepo wabaya*
3. Je, Mungu iko na nguvu juu ya roho za mapepo wabaya*? Ndiyo*
4. Shetani anawaambia watu kufanya nini wakati wanapokuwa na matatizo? *Anawaambia wajiuwe*
5. Kwa nini austahili kumusikiliza shetani hata maramoja? *Kwa sababu shetani anamuchukiya Mungu na Mwana damu na anapenda watu wapatwe na mambo mabaya*
6. Unapokuwa na matatizo ao unajuwa mutu mwenye matatizo unaombwa kufanya nini? *Kumwambia Mungu na kisha kumwambia mutu ambaye unaye mwamini*

SOMO LA 34

YESU ANA NGUVU JUU YA PEPO

SHAURI KWA MWALIMU

Vijana siku hizi wanapambana na hali zinazo leta woga. Mauwaji,ubakaji, unyanyasaji wa jinsia, fujo ni sehemu yao ya maisha. Uwakumbushe wanafunzi wako kwamba Mungu anajuwa na anajali na pia anaweza kuwakinga na hali hizo ikiwa wana muhitaji.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mwanzo 1:9 – 10	Kutoka 14:21 – 22
Yoshua 4:23 – 24	Zaburi 24: 1 – 2
Zaburi 37	Marko 4: 35 – 41

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

Uwafundishe wanafunzi fasi hii:

- Ni kitu gani kinacho kuleteya woga? Pepo? Sauti za kutisha? Watu wakipigana? Usiku wa giza? Kuwa peke yako?
- Kuko mambo mengi sana yanayo weza kutuletea woga, kila mutu kuna wakati anapata woga
- Hata wale wanafunzi 12 wa Yesu walikuwa wenye woga
- Usiku moja Yesu na warafiki yake walikuwa wakipita katika bahari kubwa , bahari hilo liliitwa bahari ya galilaya, walikuwa katika mutumbu mudogo. Hapo hapo pepo mukali ikaanza kuvuma
- Mawimbi mukumbwa ya kaanza kusukuma mutumbu wao na mutumbu ukaanza kujaa maji.

- Watu wakaanza kuogopa wakizaniya kwamba mutumbu wao utazama na hivo watamezwa na maji marefu
- Yesu naye alikuwa ndani ya mutumbu huo lakini alikuwa analala
- Kwa vile pia Yesu ni Mungu, alikuwa pia mwanadamu, alikuwa amechoka na hivo hakahitaji kulala.
- Lakini ni namuna gani angeliweza kulala katika zoruba hii ya kutisha?
- Warafiki zake walianza kumuhamusha na kumwambia: haujali hata kama tukizama sisi wote?
- Unazani Yesu aliwajali? Ni kweli alikuwa anawajali
- Watu walikuwa wamekwisha muona akiwalisha watu zaidi ya 5000, akiponya watu magonjwa, akifukuza mapepo, ilibidi wajuwe kwamba atawasaidia katika wakati huu mugumu
- Kumbuka mwanzo wa biblia katika kitabu cha Mwanzo, tunasoma kwamba Mungu aliumba dunia na bahari bila kutumia kitu chochote
- Kwa wakati wa Musa Mungu alifungua bahari iliwaisraeli watoke katika mikono ya majeshi ya wa misri
- Mungu anaweza kufanya chochote sababu yeye ndiye Muumbaji wa kila kitu
- Ana nguvu na mamulaka juu ya kila kitu, sababu kila kitu ni chake, hata bahari, upepo na mawimbi.
- Ndipo Yesu alisimama ndani ya mutumbu hule na akahamuru pepo na mawimbi hayo kutulia
- Yesu alikuwa na marafiki zake ndani ya mutumbu usiku hule na akawaokowa kuzama kutokana na upepo hule
- Hatuwezi kumuona Yesu siku hizi lakini iko pamoja nasi kama Roho mutakatifu
- Mpaka leo iko na uwezo wa kutusaidia tunapokuwa na woga ao tunapo kuwa katika matatizo
- Kumbuka Mungu anawaangalia wale watu wanao muamini katika Yesu
- Kwa hiyo siku ingine ukiwa na woga kumbuka hadisi hii na umuite Yesu akusaidie na kukulinda. Alifanya hivyo kwa wanafunzi wake atafanya hivo hivo na kwako pia.

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Zaburi 145:18

Maulizo ya uchunguzi

1. Sababu gani wana funzi wa Yesu waliogopa? *Walifikiri kwamba watazama ndani ya bahari*
2. Yesu alikuwa akifanya nini ndani ya mutumbu? *Alikuwa amelala*

3. Nani aliumba bahari? *Mungu*
4. Ni nani alifunguwa bahari ili waisraeli wapate kukimbia wa askari wa misri? *Mungu*
5. Sababu gani pepo na mawimbi vili mutii Yesu*? Kwa sababu Yesu ni Mungu na anamamulaka juu ya kila kitu*
6. Je! Mungu anaweza kukusaidia unapokuwa na woga ao unapokuwa katika matatizo? *Yesu anaweza*

SOMO LA 35

MUNGU ANAPENDA WATOTO

SHAURI KWA MWALIMU

Mungu anamujali kila mutu wakubwa na watoto katika hadisi hiyi tunaona ginsi Yesu alivyo mufufua mutoto kutoka wafu. Uwakumbushe wanafunzi kwamba hijapo kuwa bado wao ni wadogo, Yesu anawapenda na anawajali kama vile anavyo wapenda wakubwa

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Matayo 9: 27 – 31
Matayo 14:22 – 36
Matayo 19: 13 – 15
Luka 8: 40 – 56
Yoana 20: 30 – 31

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi

- Yesu alifanya miujiza mingi yenye nguvu wakati alipokuwa akiishi hapa duniani
- Aliponyesha vipofu wakaona tena, viwete wakatembeya, aliponya watu kutoka kwa magonjwa ya ngozi, alifukuza mapepo mabaya, aliwalisha watu 5000, kwa mikate tano na samaki mbili alituliza bahari na hata alitembeya juu ya maji bila kuzama
- Ni sababu gani Yesu alifanya haya yote?
- Alifanya haya kusititiza kwamba yeye ni Mungu Mwana
- Yesu alitaka watu waamini kuwa yeye ndiye ule aliye ahidiwa toka mwanzo wa dunia, ambaye alikuja kuharibu utawala wa shetani, kulipa zambi zetu na kututengenezea njia ya kurudi katika familia ya Mungu

- Siku moja Yesu alifanya muujiza ingine mukubwa
- Mutu moja aliye itwa YAIRO alikuwa na mutoto mudogo wa kike ambaye alikuwa mugonjwa sana karibu ya kufa
- YAIRO alikuwa ameisha sikia habari za Yesu na alikuwa na imani ya kwamba Yesu anaweza kuponesha mutoto wake
- Wakati Yesu alitembea kuelekea kwenye nyumba alimokuwa akiishi binti YAIRO watu wengine walikuja kumuambia Yesu kama binti yule ameisha kufa
- Walifikiri kwamba aita wezekana tena kumusaidia lakini Yesu aliendelea kwenda kwenye nyumba hile
- Yesu alipofika kila mutu alikuwa analia inje ya nyumba hiyo sababu binti yule amekwisha kufa
- Yesu akamutwa YAIRO na mama wa binti yule na wanafunzi watatu katika wanafunzi wake wakaingia ndani ya chumba alimukuwa amelazwa binti yule
- Yesu akamukamata mukono binti yule na kumuamuru aamuke
- Roho yake ikamurudilia na hapo hapo akasimama na kuanza kutembeatembea mule ndani
- Yesu akamuambia mama ya mutoto yule amupe chakula akule, akawa muzima kabisa
- Binti huyu alipendwa sana na Yesu, alimujali sana na anakujali hata na wewe pia

<u>Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.</u>

Matayo 19: 14

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Ni miujiza gani ambayo Yesu alifanya? *Kuwaponya vipofu, wagonjwa, viwete n.k*
2. Sababu gani Yesu alifanya miujiza hii? *Ili watu waamini kwamba yeye ni Mungu Mwana*
3. Kwa nini YAIRO alimuita Yesu? *Alikuwa na imani kwa Yesu kwamba anaweza kumuponya binti wake.*
4. Sababu gani watu walikuwa wanalia? *Sababu binti yake alikuwa ameisha kufa*
5. Kitu gani kilitokea Yesu alipo mugusa? *Roho yake ilimurudia na akasimama*
6. Je! Mungu anajali watu wakubwa tu? *Hapana anajali hata watoto pia*

SOMO LA 36

YESU ANATUFUNDISHA KUOMBA

SHAURI KWA MWALIMU

Maombi ni kitu cha maana kwa kuwa mtoto wa Mungu ni vizuri uwa sikilishe wanafunzi wako kutumia wakati wakiwa wenyewe na Mungu kila siku na kuendelea kusema naye kwa siku yote wanapokuwa wakitumika ao kucheza uamini kuwa na weye unafanya vile

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mizali 15:29	Mathayo 6:1-15
Luka 11:1-13	Luka 18 :1-14
Waefeso 6:18	wafilipi 4:4-7
1wathesalonike 5:16-18	1timotheo 2:1-4

Rudiliya maulizo somo la mbele pamoja na wanafunzi

Uwafundishe wanafunzi fasi hii

- Wakati yesu alipoishi hapa mudunia, aliwafundisha wanafunzi wake mambo mingi
- Walifanya hivi sababu nao wata wafundisha watu wengine
- Kitu kimoja katika yale aliyowafundisha ni ginsi ya kuomba
- Kama weye uko muamini kwa yesu, basi ujue Mungu ni Baba yako wa mbinguni
- alipenda kusema na weye, na anapenda vilevile weye useme naye, kama vile inavyo zungumuza na wazazi wako ao warafiki yako kila siku
- Anayesema na sisi wakati tunaposoma Biblia neno lake na kwa njia ya roho mutakatifu katika roho zetu

- Tunasema na Mungukuhusu kila kitu mwambie kama unashida ya warafiki wa kucheza nao umwambie kama unasikia njala ao unasikia vibaya katika mwili wako, mwambie kama uko na matatizo kunyumba ao kumasomo, ao umwambie akuponye kama uko mgonjwa
- Unaweza kuomba Mungu kila saa yote ile, iwe usiku au muchana chini, umesimama una piga magoti ao una lala chini wakati wa kuomba Mungu hajali ni ginsi gani
- Mungu hatoi majibu ya maombi yetu kwa ginsi tulivyo muomba, kwa sababu mara nyingi tuna muomba kwa nia mubaya.
- Mara nyingi Mungu anasema "Ndiyo" kwa maombi yetu, na wakati ungine anasema "hapana" ao wakati ungine anasema "ngoja"
- Ni churti tujifunze kumwamini Mungu na kujua kama atatupatia vitu vizuri kwetu
- Vile unavyosema na Mungu, ni vile pia utajifunza mingi kwake kwa ginsi atakuwa anajibu maombi yako hiyi ndio sababu kubwa ya maana yako kuomba kila siku.
- Mara nyingi inakuwa vigumu kwetu kujua namna ya kuomba na tuombe Mungu kitu gani
- Yesu alitupa mufano muzuri wa kufuata kutusaidia tunapotaka kuomba tunaiita " sala ya Bwana"
- Anza maombi yako kwa kumutukuza Mungu kwanza kisha muombe kazi yake na mapenzi yake yatimizwe hapa duniani
- Na kisha hapo uombe kitu unacho itaji ili uhishi
- Kisha uwasamehe wale wote walio kukoseya. Kumbuka kwamba Mungu anakusamehe na wewe pia makosa yako yote uliyo tenda
- Kisha uombe Mungu akusaidie kumutii katika kila kitu na kukulinda na yule muovu shetani
- Mwisho umusifu Mungu sababu Mungu ni mukuu sifa na utukufu ni vyake
- Yesu anasikia na anajibu maombi yote ya watoto wake hivo usikate tamaa endelea kumuomba Mungu anasikia

Vesi za kukumbuka ambazo mwalimu atafundisha wanafunzi kisha somo akitumikisha mwenendo wa kusisimuwa.

Wafilipi 4: 6

Maulizo ya uchunguzi

1. Ni vitu gani unaweza kumuomba Mungu? Chochote
2. Wakati gani unaweza kumuomba Mungu? Wakati wowote
3. Wakati wa kuomba ni sherti kupiga magoti? Hapana
4. Je! Mungu anajibia maombi kwa namna tunavyo muomba? Hapana
5. Sababu gani ? Mungu anatupatia vitu ambavyo ni vizuri, kwetu

6. Je! Mungu anajibu maombi yetu kila wakati? Ndiyo, wakati moja" ndiyo" wakati ungine anasema "hapana" na wakati ungine anasema "ngoja"

SOMO LA 37

UKWELI KUHUSU VIRUSI VYA UKIMWI (sehemu ya 1)

SHAURI KWA MWALIMU

Mamilioni ya watu wanakufa juu ya virusi vya ukimwi mu dunia yote ni shurti uwaambie wanafunzi wako ukweli juu ya ugonjwa huyu wa hatari ili wanafunzi wako waweze kufanya uchaguzi ya akili katika maisha yao na waweze kuishi huru kutoka kwa ugonjwa huu wa kuleta boga.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Luka 5:12-13 Luka 17:11-19

Rudilia maulizo ya somo la mbele pamoja na wanafunzi

Uwafundishe wanafunzi fasi hili

- Yesu aliponya magonjwa mengi alipokuwa hapo mu dinia
- Kila mutu aliyekuja kwake na akiamini kuwa Yesu atamponya, basi alipona na kurudishiwa afya yake.
- Yesu haku mufukuza hata mutu mumoja, aliye kuja kwake, bila kujali ni ugonjwa wa ginsi gani aliyo nayo.
- Siku moja, wanaume 10 waliokuwa na ugonjwa wa hatari wa ngozi (unaoitwa ukoma) walitaka kuponyeshwa na yesu

- Hawa watu walikuwa wanaishi mbali na jamaa zao na warafiki sababu huu ugonjwa ungeweza kuambukia kutoka kwa mutu mumoja kwenda kwa mwengine.
- Yesu alijua ni upweke gani na ni uzuni gani walikuwa nayo hivi alifika na kuwaponya wote.
- Watu walikuwa wanaogopa sana ugonjwa huu wa ukoma, na leo hii kuko ugonjwa ungine ambao watu wanaogopa saana unaitwa Ukimwi.
- Ukimwi pia unaweza kuambukia kutoka kwa mutu mumoja kwenda kwa mwingine ila huu ugonjwa ni tafauti na ukoma
- Hauwezi kupata ukimwi kwa kugusana na mutu ambaye iko na ugonjwa ao kwa kumukumbatiya mutu ambaye iko na ukimwi
- Hauwezi kupata ukimwi kwa kuchangiya chumba ao kabine (w.c.) moja ao kwa kuchangia saani na vijiko.
- Kuko njia 3 kubwa ambazo ukimwi unaweza kuambukizwa kutoka kwa mutu moja kwenda kwa ungine.
    1. Mama wa mimba anaweza kuambukiza mtoto ambaye ajazaliwa
    2. Ikiwa damu ya mugonjwa wa ukimwi itagusana na mutu ambaye hana ukimwi , basi huyu naye atapata ukimwi hiyo pia inaweza kutokea kama unachangia wembe wakati wa kumnyoa ama kama muganga atatumia kisu kile kufanya yando
    3. Kufanya ngono na mutu ambaye tayari amekwisha kuambukizwa ni hatari sana na watu wengi wanapata virusi vya ukimwi kwa njia hii.
- Mutu wa ukimwi ataanza kupata magonjwa tafauti kama , mafua, kikohozi, upele kwenye ngozi, kuhara, kupunguka kilo, homa, kifua kikuu mara kwa mara.
- Kiisha miaka kidogo watu hawa wanagonda na kufa
- Ukimwi ni ugonjwa wa hatari sana na hakuna muganga ambaye ameisha pata dawa ya kuponya ukimwi.
- Mungu hapendi mutu yote apate ukimwi, ao kufa kwa ukimwi.
- Kwa somo linalo fuata hili, tutajifunza neno la Mungu kujua mpango wa Mungu kwa maisha yetu ili tuweze kukingiwa na ugonjwa huu wa ukimwi

<u>Vesi za kukumbuka za kuwafundisha mpango wa mipangilio kisha somo</u>.

Yohana 8:32

1) Ni ugonjwa gani wa ngozi ambao wale wanaume 10 walikuwa nao? *Ukoma*
2) Sababu gani watu waliogopa ugonjwa wa huu? *Sababu ulikuwa unaweza kuambuzwa kutoka kwa mtu moja kwenda kwa mutu ungine*
3) Je, unaweza kupata virusi vya ukimwi kwa kuchangiya chumba na mtu wa ukimwi? *Hapana*
4) Ni njia 3 za namna gani ambazo zinaweza kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi? *Mama wa mimba mwenye iko na virusi vya ukimwi anaweza*

kuambukiza mtoto wake, damu yenye virusi vya ukimwi kwa damu ingine, tendo la ngono na mtu mwenye ukimwi

5) Ni magonjwa gani ambayo mutu wa ukimwi anayapata? *Magonjwa ya ngozi, kuharisha, kupoteza uzito, kifua kikubwa n.k.*
6) Je kuko dawa yote inaweza kuponya ukimwi? *Hapana.*

SOMO LA 38

UKWELI KUHUSU VIRUSI VYA UKIMWI (sehemu ya II)

SHAURI KWA MWALIMU

Kwa wakati wa Agano la kale Mungu aliwaruhusu watu kuwa na wanawake wengi kuzidia mumoja Agano jipya linafundisha kuwa ni mubaya kukosa adabu katika mapendo yaani kuwa na mwanamuke zaidi ya mumoja kama vile hatuendelee tena kutowa sadaka za nyama sababu ya kupata musamaha wa zambi, njoo hivo hatutaendelea kufuata mifano ya Agano la kale kuhusu mapendo ya ndoa.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Mwanzo 16:1-4
1Wafalme 11:1-6
1Wakorintho 6:9-20
1Wakorintho 10:12-13
Mwanzo 26:16-30
Yohana 8:44
1Wakorintho
2Petro 2: 4-9
Mathayo 19:1-9

Uwafundishe wanafunzi fasi hii:

- Kwa somo letu lililopita tumejifunza njia ambazo watu wanaweza kuambukizwa ukimwi, Na vitu vinavyotokeea wakati wanapo ambukizwa.
- Tulisema kuwa Mungu hapendi mutu yote kupata ugonjwa huu
- Mungu ametupatiya maagizo kutoka neno lake (Biblia) ambayo Yana tukinga na ukimwi kama tutayaheshimu.
- Maagizo ya Mungu siyo nguvu kuyaheshimu Kwa sababu ametupatia roho mutakatifu kutusaidia kushinda majaribu Na kutusaidia kumuheshimu Mungu.
- Mungu anajuwa kila kitu kizuri Kwa maisha yetu Na Ni lazima kusikia maagizo yake Kwa ajili ya kujikinga.
- Tumekwisha kusema kuwa njia kubwa ambayo watu wanaambukizwa ukimwi Ni tendo la ngono Na mutu mwenye virusi vya ukimwi.
- Vijana mingi, hata wenye miaka 12 na 13 watoto, wakubwa, wanafanya tendo la ngono wanazania kuwa ni vizuri ni huru kwa kila mtu kufanya vile.
- Hiyo siyo kweli kabisa, shetani anawadanganya vijana ili wamuamini.
- Television, simema, muziki, magazeti hivi vyote vinadanganya uongo wa shetani kuhusu kufanya ngono na wapenzi wengi.
- Kama uko na wapenzi wengi kuko urahisi mukubwa kabisa wa kupata ukimwi hata kama unafanya na mpira (kondom).
- Mpira (kondom) haina uhakika wa asilimia 100(100%) kukinga ukimwi.
- Mpango wa mungu kwa watoto wake ni kwamba wakomale na kuchagua mwanamuke ao mwanamume wa kikristo wa oane hao wafanye tendo la ngono kila moja na mupenzi wake tu.
- Ikiwa mwanaume ao mwanamuke watafanya hivi, hawawezi kupata virusi vya ukimwi.
- Sasa umekwisha kusikia mupango wa Mungu kuhusu ndoa na mupenzi: kama utachagua kutokumuheshimu Mungu kwa hivo, unaweza kupata virusi vya ukimwi nakufa mbele ya kufikia myaka 20.
- Jibu la Mungu kuhusu ukimwi ni nini ? **mwanaume umoja, mwanamuke mumoja kwa maisha yote**

<u>Vesi za kukumbuka za kuwafundisha wanafunzi pango wa mipangilio baada somo.</u>

<u>1 wakorintho 6 : 18 (sehemu ya kwanza)</u>

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1) Ni nani aliyekuja kutusaidia kuepuka majaribu ? *Mungu roho mutakatifu*.
2) Je, tunaweza kuheshimu maagizo ya Mungu ? *ndio*
3) Ni nani anawaruhusu watu kwamba wapenzi wengi ni vizuri ? *shetan*i
4) Je, mpira (kondom) inaweza kukukinga na ukimwi kila wakati ? *hapana.*

5) Ni wakati gani unaruhusiwa kufanya mapenzi ? *kisha kuowa ao kuolewa.*

SOMO LA 39

BILA KUWA NA YESU, HATUWEZI KUMPENDEZA MUNGU

SHAURI KWA MWALIMU

Yesu ndiye jia ya kweli, jia zetu sisi wenyewe siyo za kweli. Hatuwezi kujiokowa sisi wenyewe na hukumu ya zambi. Ni kwa kuamini yesu tu, hapo tunaweza kupata uhakika upendo wa yesu ili Mungu atupokee kama watoto wake.

Vesi za biblia kwa mwalimu mbele ya kufundisha:

Isaya 61 : 10
Warumi 3 : 23
Wrumi 10 : 1-4
Wagalatia 3 : 6-14
Waefeso 2 : 8-9
Mathayo 5 : 17
Warumi 6 : 23
2 wakorintho 5 : 20-21
Wagalatia 3 : 21-25
1 petro 3 : 18

Rudilia Maulizo ya somo la mbele

- Mungu alipatia musa amri zake, miaka 1500 mbele ya yesu, mkombozi lazima kuja kuishi mu dunia.
- Musa aliandika amri hizo na zikapitishwa kizazi hadi kizazi.

- Watu wengi wa wakati wa yesu, walikubali kwamba kwa kujaribu kuziheshimu hizi amri Mungu atawapenda na atawakubali kama watoto wake.
- Hawakufahamu kwamba haiwezekanikukubaliwa na Mungu kwa kuheshimu sheria.
- Watu wote tumezaliwa kwa Adamu wanazaliwa wakiwa na zambi, na hivyo wametenganishwa na Mungu.
- Tunapakosea wazazi wetu heshima, kufikiri mambo mabaya, kudanganya, kutetana, kuiba vitu n.k "Mme moja – mwanamuke moja" kwa maisha yote. Mambo yote haya yanahakikisha kwamba tumezaliwa tukona zambi.
- Ni sherti sote tuhukumiwe katika ziwa la moto
- Tunahaja na mutu wa kutuakowa kutoka kwa mamulaka ya shetani, kulipa zambi zetu, na kuturudisha katika jamaa ya mungu.
- Yesu ndiye mutu wa kipekee aliye heshimu kwa ukamilifu amri za mungu.
- Yesu alimuheshimu Mungu baba kikamilifu kwa kila njia kwa sababu hakuzaliwa kwa Adamu kama sisi, alitoka kwa Mungu.
- Yesu aliwaambia waalimu kwamba hakukuja kuvunja amri za musa, lakini alikuja kuzitimiza kwa kuziheshimu kikamilifu.
- Hatuwezi kujigomboa wenyewe kwa kujaribu kujifanya wazuri, tunamuhitaji yesu kutuokoa
- Tunapokuwa na Imani naye, basi nzuri na uhaki za yesu zinakuwa zetu na hapo Mungu anatutazama kama wakamilifu, tusiokuwa na uchafu na tuliosamehewa.
- Tuna kushukuru Mungu kwa kumutuma yesu, mkombozi aliyeahidiwa kwa sababu bila yesu hatuwezi kumupendeza Mungu vyakutosha.

<u>Vesi za kukumbuka za kuwafundisha wanafunzi kwa mpango wa mipangilio baada ya somo.</u>

<u>Warumi 6 : 23</u>

<u>Maulizo ya uchunguzi</u>

1. Sababu gani tunazaliwa wenye zambi ? *kwa sababu sote tumezaliwa kwa Adamu.*
2. Ni mambo gani tunayofanya yanayo hakikisha kwamba tumezaliwa tukiwa na zambi ? *kusema wongo, kuiba, kutetana. N.k*
3. Ni mutu gani aliye hesimu amri zote za Mungu ? *yesu.*
4. je, yesu alikuja kuvunja amri ambayo musa alipewa na Mungu ? *hapana alikuja kuzitimiza*.
5. je, zambi zako zinasamehewa kwa kuheshimu amri za Mungu ? *hapana.*

6. Ni njia gani ya kipekee inayo kuwezesha kusamehewa zambi zoko *? kwa kuamini kwamba yesu alichukua hukumu ya zambi zako.*

SOMO LA 40

TUNASTAHILI KUPENDANA

SHAURI KWA MWALIMU

Kama tukisema sisi ni wa kristo ni sherti matendo yetu ya kamilishe hivyo tuta onyesha namuna gani upendo wutu kwa Mungu ? Ni kwa kuwapenda watu wengine kama hatuwapendi watu wengine hatuwezi kumupenda Mungu.

Maandiko matakatifu ambayo mwalimu anastahili kujua mbele ya kufundisha.

Marko 12 :28 -34
Yohana 13 :34-35
Waefeso 4 :22-32
1Yohana 2:3-6
1Yohana 4:7-12
Luka 10 :25-37
Matendo ya mitume 10 :34-35
Yeremia 2
1Yohana 3:11-18
1Yohana 4:19-21

Rudilia maulizo ya somo lililopita pamoja na wanafunzi:

wafundishe wanafunzi fasi hii ;

- Kwa somo lililopita,tulionyesha kuwa Yesu hakuja kuzivunja sheriya ambazo Musa alipewa.
- Yesu alikuja kuziheshim na kutusaidia sisi kuzijuwa vizuri.
- Sikumoja, sehemu ya waalimu wa sheriya walimujaribu Yesu,ili waone kama anazijuwa sheriya alizozipewa Musa.
- Waka muuliza 'ni amri gain iliyo kubwa'?
- Yesu akawajibu'Umupende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na umupende jirani yako kama mwili wako'
- Wakati ungine,Muyahudi na mwalimu wa sheriya,walimuuliza Yesu ulizo lingine.
- Akasema, jirani yangu ni nani?
- Pengine huyu mutu alikuwa na shida ya kuwapenda sehemu ya watu,ao pengine alitaka kujuwa kama anaombwa kuwapenda wale tu anayeishi karibu naye,ao familia yake na warafiki zake tu.
- kwa ku mujibu huyu mutu,Yesu alimwambia habari hii.
- Kulikuwa na muyahudi moja aliye kuwa ana safiri , akipita njia hiyo mara wa mwizi waka mukamata , wakamuvula manguo wakamwiba pesa na kumuumiza vidonda.
- Wakamuacha analala kwa njia hiyo karibu na kufa.
- Mara moja kuhani akapita kwa njia hiyo,alipomuona alipita pembeni ya njia na akaendelea.
- Mulawi naye akapita kwa njia hiyohiyo, naye pita hakumusaidia.
- Mara moja Musamariya akapita kwa njia hiyo.
- Wasamariya walikuwa watu wenye kuchangamana na walikuwa ni wayahudi ambao waliowa wanawake wa kabila zingine.Waliishi kwenye muji wao na vijiji vyao.
- Wayahudi walichukiana na wasamariya, kwa sababu walizania kwamba wao ni wema kupita wasamariya.
- Yule musamaria alisimama ili amusaidiye.
- Kwa sababu gani Yesu aliwaambia habari hiyo ?
- Yesu aliwaambia kwamba Musamariya alikuwa anajuwa kama anachukiwa na Muyahudi lakini alimuhurumiya , akasimama akamusaidia.
- Yesu alisema kwamba Mungu anapenda sisi tuwapende na kuwaheshimu kila mutu, hata kama ametokea kabila gani inchi gani anaishi namuna gani ana rangi gani ao ni wa dini gani.
